BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TATHMINI YA WATAHINI KUHUSU UFAULU WA WATAHINIWA WA KIDATO CHA NNE, 2014

015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TATHMINI YA WATAHINI KUHUSU UFAULU WA WATAHINIWA WA KIDATO CHA NNE CSEE, 2014

ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2015

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO

DIBAJI iv
1.0 UTANGULIZI 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA 2
2.1 KARATASI YA KWANZA 2
2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi 2
2.1.2 Swali la 2: Qur'an 3
2.1.3 Swali la 3: Tawhiid 4
2.1.4 Swali la 4: Fiqh 5
2.1.5 Swali la 5: Tarekh 6
3.0 KARATASI YA PILI 7
3.1 SEHEMU A: QUR'AN 7
3.1.1 Swali la 1: Sura Zilizoteuliwa 7
3.1.2 Swali la pili: Qur'an ni Neno la Allah (s.w) 10
3.1.3 Swali la 3: Sura Zilizoteuliwa. 14
3.2 SEHEMU B: TAWHIID 18
3.2.1 Swali la 4: Dini Sahihi 18
3.2.2 Swali la 5: Shirk 22
3.2.3 Swali la 6: Nguzo za Imani 26
3.3 SEHEMU C: FIQH 30
3.3.1 Swali la 7: Nguzo za Uislamu (Swala) 30
3.3.2 Swali la 8: Ndoa katika Uislamu 34
3.3.3 Swali la 9: Swala ya Maiti 37
3.4 SEHEMU D : TAREKH 41
3.4.1 Swali la 10: Historia ya Uislamu Kipindi cha Makhalifa Wanne Waongofu 41
3.4.2 Swali la 11: Mkataba wa Hudaibiyah 46
3.4.3 Swali la 12: Dhana ya Uislamu juu ya Historia 51
4.0 HITIMISHO 57
5.0 MAPENDEKEZO 58
Kiambatanisho 59

DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kidato cha Nne 2014 kwa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakaguzi, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi na walioshindwa kujibu kwa usahihi. Uchambuzi huu umeonesha jinsi watahiniwa walivyopata alama za juu, kati na chini kwa kila swali na sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri au vibaya zimeoneshwa.

Taarifa hii inaonesha sababu mbalimbali ambazo zilichangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Uchambuzi uliofanyika unaonesha watahiniwa walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na kutotambua matakwa ya maswali na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali za somo hili. Aidha, kuna udhaifu mkubwa katika kuhifadhi na kutafsiri Qur'an na Hadithi za Mtume (s.a.w).

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupata ufumbuzi wa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wahitimu wa Kidato cha Nne katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kidato cha Nne hasa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mratibu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, walimu, Makatibu Muhtasi na wengine wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) wa mwaka 2014 kwa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu uliofanyika November 2014 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo hili kwa Kidato cha I – IV. Mtihani huu ulikuwa na karatasi mbili; karatasi ya kwanza ilikuwa na sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali matano ya majibu mafupi (Objective Questions) ambapo watahiniwa walitakiwa kuyajibu maswali yote. Maswali haya yalikuwa na jumla ya alama 100. Karatasi ya pili iligawanyika katika sehemu A, B, C na D. Kila sehemu ilikuwa na maswali matatu ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja kutoka kila sehemu. Kila swali lilikuwa na alama 25 ambapo jumla ya alama ilikuwa 100.

Jumla ya watahiniwa 30,300 waliandikishwa kufanya mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwaka 2014. Kati ya hao, watahiniwa 28,943 walihudhuria kufanya mtihani huu. Hii ni pungufu ya watahiniwa 6,966 ukilinganisha na watahiniwa 35,909 waliofanya mtihani wa Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwaka 2013. Watahiniwa 7,683 sawa na asilimia 26.6 ya watahiniwa waliofannya mtihani huu walifaulu ambapo mtahiniwa 1 alipata A, watahiniwa 125 walipata B+, watahiniwa 916 walipata B, watahiniwa 3,512 walipata C na watahiniwa 3,129 walipata D. Watahiniwa 21,260 sawa na asilimia 73.4 walifeli, ambapo watahiniwa 12,470 walipata E na watahiniwa 8,790 walipata F. Kwa ujumla ufaulu wa mwaka 2014 umeshuka kwa asilimia 14.4 ukilinganisha na matokeo ya mwaka 2013.

Taarifa hii inaelezea uchambuzi wa maswali ya mtihani na majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Sampuli za majibu ya watahiniwa pia zimewekwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na watahiniwa. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ya vizuri, wastani na hafifu kutegemea na wastani wa asilimia ya watahiniwa waliopata asilimia 30 na zaidi ya alama zilizopangwa kwa swali husika. Mada ilikuwa na ufaulu hafifu kama asilimia ya watahiniwa waliopata wastani wa asilimia 30 na zaidi ni alama 0 hadi 29, kutoka alama 30 hadi 49 ufaulu wake ulikuwa ni wastani na kutoka alama 50 hadi 100 ufaulu wake ulikuwa ni mzuri.

Inatarajiwa kwamba kupitia uchambuzi uliooneshwa katika taarifa hii

ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi walioko shuleni na wale wa kujitegemea utaimarika zaidi na hivyo kupandisha ufaulu wa watahiniwa wajao katika somo hili.

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA

2.1 KARATASI YA KWANZA

2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi

Swali hili lilikuwa na vipengele kumi (i - x) na lilitahini mada za Sunnah na Hadithi ambazo zilikusanya maana ya Hadithi, maana ya Sunnah, Kuhifadhiwa kwa Hadithi wakati wa Mtume (s.a.w), umuhimu wa Sunnah na mada ya Maimamu Sita Waandishi wa Hadithi. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi katika majibu matano (A - E) aliyopewa katika kila swali. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 95 ya watahiniwa wote walijibu swali hili, ambapo asilimia 1.3 ya watahiniwa hao walipata alama 0, asilimia 28.3 walipata alama 1 hadi 2, asilimia 70.4 walipata alama 3 hadi 8.

Ufaulu wa jumla katika swali hili kwa watahiniwa ulikuwa ni wa wastani kwa sababu wengi walipata alama 3 hadi 6. Watahiniwa waliopata alama za juu kwenye swali hili walionekana kuwa na maarifa ya kutosha katika mada za Sunnah na Hadithi, hivyo kujibu swali hili kwa ufasaha. Watahiniwa walio wengi waliweza kufanya vizuri zaidi katika kipengele cha (ii), (iii), (v) na (x). Hii inatokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizotahiniwa katika vipengele hivi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walishindwa kufanya vizuri katika baadhi ya vipengele hasa cha (vi), (vii) na (viii). Watahiniwa hao walichagua majibu kwa kubahatisha bila ya kuwa na maarifa kwenye mada za vipengele hivyo. Kwa mfano, katika kipengele cha (vi) watahiniwa wengi walichagua B badala ya A kwa kuwa majibu haya kwa kiasi kikubwa

yalikaribiana. Aidha, katika kipengele cha (vii) watahiniwa walichagua zaidi jibu C na D badala ya jibu sahihi B. Katika kipengele cha (viii) watahiniwa walichagua zaidi jawabu D badala ya C kwa sababu neno 'dhaifu' liliwavutia zaidi kwa vile limezoeleka sana katika istilahi ya aina za Hadithi badala ya neno 'maudhuu' ambalo lilikuwa jibu sahihi.

2.1.2 Swali la 2: Qur'an

Swali lilihusu mada ya Qur'an na lilikuwa na vipengele 15 ambapo mtahiniwa alitakiwa kuoanisha vifungu vya maneno katika vipengele vya Orodha A (i - xv) na vile vya Orodha B (A - T) na kuandika majibu yake katika kitabu cha kujibia. Kila kipengele kilikuwa na alama 1, ambapo jumla ya alama zote za swali hili zilikuwa 15.

Asilimia 94.9 ya watahiniwa wote walijibu swali hili, ambapo asilimia 3.9 ya watahiniwa hao walipata alama 0, asilimia 55.5 walipata alama 1 hadi 5 na asilimia 40.6 walipata alama 6 hadi 14.

Ufaulu wa watahiniwa kwa ujumla ulikuwa wastani. Watahiniwa walio wengi walifanya vizuri katika vipengele (iii), (iv), (v), (viii), (xii), (xiii), na (xiv). Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sura Zilizoteuliwa na pia kubaini ujumbe wa aya za Qur'an na hivyo kuweza kuaonisha vizuri vifungu vilivyoko katika orodha A na vile vilivyoko katika orodha B**.**

Watahiniwa wachache walikuwa na ufaulu hafifu katika swali hili. Watahiniwa hao walijitengenezea mtindo wa aina tofauti wa uwasilishaji wa majibu jambo lililosababisha kukosa alama. Kwa mfano, kuandika kwanza herufi iliyo katika kifungu B na kisha kuorodhesha mbele yake vifungu kadhaa kutoka A vinavyowiana na kifungu hicho (A = ix, xv), (B = v, viii, xi)**.** Mfumo huu wa kuandika majibu mengi kwa kipengele kimoja, badala ya herufi moja ya jibu kwa kila kipengele kama swali linavyoelekeza, ulisababisha watahiniwa hawa kukosa alama. Baadhi ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kwani

waliandika majibu yasiyo sahihi kwa vipengele vingi vya swali hivyo kupata alama chache. Baadhi ya vipengele ambavyo watahiniwa hawakuweza kufanya vizuri ni (i), (ii), (ix) na (x).

2.1.3 Swali la 3: Tawhiid

Swali lilihusu mada za Tawhiid na mtahiniwa alitakiwa kuzipanga sentensi katika mtiririko wenye kuleta mantiki katika vipengele (a), (b), na (c) ambapo kila kipengele kilikuwa na sentensi tano (i - v). Kipengele (a) kilijumuisha sentensi tano tofauti za hoja za Makafiri juu ya kuwepo kwa Allah (s.w). Kipengele (b) kilihusu madai ya makafiri dhidi ya ufufuo. Kipengele (c) kilihusu aya zinazohusu adhabu itakayowapata watu wanaofuata upotofu baada ya kuwajia haki hapa duniani. Kila kipengele kilikuwa na alama 5 na jumla ya alama zote za swali hili zilikuwa 15.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 93.1 ya watahiniwa wote, ambapo asilimia 36 walipata alama 0, asilimia 52.5 walipata alama 1 hadi 5.5 na asilimia 6.1 walipata alama 6 hadi 14.

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa dhaifu. Katika vipengele vyote vitatu watahiniwa walio wengi hawakufanya vizuri. Watahiniwa walishindwa kuzipanga sentensi kwa usahihi kwa sababu walikosa maarifa ya upangaji wa sentensi hasa aya za Qur'an na kusababisha watahiniwa wengi kupata alama 0 (asilimia 36). Pia kuna baadhi ya watahiniwa hawakufuata maelekezo hivyo kujibu kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, katika kuzipanga sentensi baadhi walitumia namba (1, 2, 3) na wengine walitumia herufi (a, b, c) katika majawabu yao, mpangilio ambao haukuwa sahihi. Swali lilielekeza kuzipanga sentensi kwa kutumia namba za kirumi (i, ii, iii).

Watahiniwa wachache waliweza kufanya vizuri na kuonesha kuwa na maarifa ya kutosha katika kuhifadhi Qur'an hivyo waliweza kuzipanga aya zote kwa usahihi hasa katika kipengele (b) na (c).

2.1.4 Swali la 4: Fiqh

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kujibu kwa ufupi vipengele kumi na vitano (a - o) vilivyomo katika swali hili. Swali lilihusu mada za Fiqh ambazo ni Uongozi katika Uislamu, Twahara, mambo yanayopaswa kufanyiwa maiti muislamu, vyanzo vya sheria katika Uislamu, nguzo za Uislamu (zakat), Kusimamisha Swala (Swala ya Ijumaa), Funga ya Ramadhani, Hija (Umra, maandalizi ya hija na utekelezaji wa hija), Ndoa katika Uislamu na Mirathi. Kila kipengele kilikuwa na alama 2 ambapo jumla ya alama katika swali hili ni 30.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 94.5 ya watahiniwa wote ambapo asilimia 0.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 25.6 walipata alama 0.5 hadi 8, asilimia 70.1 walipata alama 9 hadi 20, asilimia 3.7 walipata alama 21 hadi 29.5.

Ufaulu wa watahiniwa kwenye swali hili ni mzuri ambapo watahiniwa wengi waliweza kujibu vipengele vingi kwa ufasaha. Mada nyingi za swali hili kama vile Swala, Zaka, Funga, Hija na Ndoa zinatekelezwa kwa vitendo hivyo kuwafanya watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha. Vipengele ambavyo watahiniwa walifanya vizuri ni 4 (e) (h) na (n).

Baadhi ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Fiqh. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa istilahi zilizotumika katika baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama za chini. Vilevile, kutosoma vizuri na kuelewa mzizi wa swali kulisababisha watahiniwa wengi kuandika majibu yaliyo kinyume na swali lililoulizwa. Kwa mifano, katika swali la 4 (a), badala ya kuelezea wajibu wa kiongozi wa Dola ya Kiislamu, wao walitoa sifa za kiongozi wa Dola ya Kiislamu. Pia katika kipengele 4 (l), kilichouliza masharti mawili yaliyowekwa katika Qur'an kuhusu ruhusa ya kuoa mke zaidi ya mmoja, watahiniwa wengi waliandika masharti mengine yaliyowekwa nje ya Qur'an kinyume na maelekezo ya swali. Aidha, katika kipengele cha 4 (i), watahiniwa wengi walishindwa kuelewa kuwa walitakiwa kutoa sifa mbili za

ziada, japokuwa kuna sifa anazotakiwa kuwa nazo ili kuweza kwenda hija akiwa mwanaume au mwanamke. Watahiniwa walitakiwa wataje sifa sita za ziada za mwanamke anayetaka kwenda hija, kinyume chake wakataja sifa za jumla na kutoa majibu kama vile awe ni mwenye uwezo, awe na chumo halali. Kutokuelewa matakwa ya swali kwa watahiniwa pia kumeonekana katika 4 (n) ambapo baadhi ya watahiniwa waliijibu kinyume na kilichoulizwa. Badala ya kueleza mambo gani wazazi wafanyiwe na watoto wao, watahiniwa wengi walieleza mambo ambayo yanapaswa watoto wafanyiwe na wazazi wao.

2.1.5 Swali la 5: Tarekh

Swali lilihusu mada za Tarekh na mtahiniwa alitakiwa kuchagua neno au kifungu cha maneno (i) – (xxx) ili kukamilisha kauli (a-o) kwa usahihi. Mada za Tarekh zilizotahiniwa ni Dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w), Dola ya Kiislamu wakati wa Maswahaba, Historia ya Uislamu wakati wa Nabii Ibrahim, Historia ya Nabii Adam (a.s), Historia ya Mtume Muhammad (s.a.w) Makka, Watu wa Madiyan, Historia ya Nabii Ibrahim (a.s), Watu wa Nabii Swaleh (Thamuud), Dola ya Kiislamu wakati wa Khalifa Othman, Hijra, Dola ya Kiislamu wakati wa Ukhalifa wa Ali, Historia ya Uandishi wa Hadithi wakati wa Tabiin na Harakati za kuhuisha Uislamu Duniani. Swali lilikuwa na vipengele 15 na kila kimoja kilikuwa na alama 2 ambapo jumla ya alama zote za swali hili ni 30.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 94.4 ya watahiniwa wote, ambapo asilimia 1.6 ya waliofanya swali hili walipata alama 0, asilimia 51.7 walipata alama 1 hadi 8. Aidha asilimia 45.1 walipata alama 9 hadi 20, na asilimia 1.5 walipata 21 hadi 29.

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani. Vipengele vingi vilikamilishwa kwa usahihi na hivyo watahiniwa wengi walipata alama za juu. Hii inaashiria kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizoulizwa katika vipengele hivi.

Kwa upande mwingine, vipengele vya ‘n’ na ‘o’ havikujibiwa vizuri ambapo watahiniwa wengi walichanganya majibu kwa jibu la ‘’n” wakaweka “o” na jibu la “o” wakaweka “n”. Hii ilitokana na watahiniwa kushindwa kusoma kwa uangalifu na hivyo kushindwa kutofautisha vikundi vya Ikhwaanul-Muslimiin na Jamiatil-Islamy, hivyo kuwafanya watahiniwa kushindwa kuoanisha majibu sahihi ili kukamilisha maneno au vifungu vya maneno katika vipengele hivyo ili yalete maana.

3.0 KARATASI YA PILI

3.1 SEHEMU A: QUR’AN

3.1.1 Swali la 1: Sura Zilizoteuliwa

Swali lilihusu mada ya Sura zilizoteuliwa na lilipima ufahamu wa mtahiniwa juu ya kutumia tafsiri ya Surat Tyn ili kufafanua mambo yanayoonesha kutukuka na kudunishwa kwa mwanadamu na lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 10 tu ya watahiniwa wote ambapo asilimia 22.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 65.6 walipata alama 0.5 hadi alama 7 na asilimia 11.6 ya watahiniwa walipata alama 8 hadi 22.

Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo hayakuchaguliwa na watahiniwa wengi na hivyo ufaulu wake haukuwa mzuri kwani ni watahiniwa wachache waliopata alama za juu. Watahiniwa hao waliweza kuelezea nukta zenye kuonesha kutukuka na kudunishwa kwa mwanadamu. Pamoja na kutaja nukta hizo, maelezo yao hayakujitosheleza kwa nukta zote hivyo hawakuweza kupata alama zote za swali. Kielelezo 1.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali lakini maelezo yake hayakuwa ya kina kumwezesha kupata alama zote 25.

Kielezo 1.1

I Mambo matano yanayoonesha kutukuka na kudunishwa kwa mwanaadamu.

Katika suratul Tyn Allah (s.w) ameyaonesha mambo mbali mbali ambayo mwanaadamu ~~ame~~ kutukuka na kudunishwa kwa ~~keke~~. Mambo hayo ni kama yafuatayo

Kwanza mwanaadamu ametukukiwa na Allah (s.w) kwamba ata kapofanya mambo mema hapa duniani basi atamlipa mambo mema huko Akhera na atampa kila anacho kitaka huko Akhera.

Pili, Mwanaadamu alapandishwa daja

I na Allah (s.w) kwa mambo mema aliyo yafanya na huo utakuwa ni ujira wake aliyo ufanya hapa duniani na pia ujira huo utakuwa ~~wa~~ usio kwisha na ltaendelea maisha.

Tatu, Mwanadamu atakuwa ameandaliwa pepo iliyokuwa nzuri zaidi kama ata mridhisha Allah (s.w) na matendo yake mema ata kayo yafanya hapa duniani na Mlmungu kuridhika nayo na kuyafurahia na pia ataanza kukulipa hapa hapa duniani kwa hayo mema yako ulio yafanya.

Nne, Mwanaadamu uta kuwa uko katika hasara na mwenye Gonzi Munga ata kuchukia siku zote kama hutaki kufuata taratibu aliyo ziweka hapa duniani na pia maisha ya hapa duniani utayajutia na ya huko Akhera pia utayajutia mara mbili zaidi maana huko ~~utakuwa~~ kama radisha diini kuliko walio diini".

Tano, Pia mwanaadamu ata dunishwa pale ata kapofanya maovu na Mlmungu hata kuwa pamoja na yeye na mtu huyo adhabu yake ni "jahanam" moto ulio mkali sana ata kwenda kutiwa humo bila ya kwonewa huruma na mtu yoyote.

Sita, Vile vile mwanaadamu ata dunishwa na Allah (s.w) kwa madhambi mengi aliyo yaduma na pia adhabu ita mkutia kaburini na adhabu ya kaburini ni kali sana na pia Akhera ina msubiri adhabu nyengine na pia yeye udie ukosa zaidi kuliko wengine wenye makosa kuliko yake kama iliyo bainishwa katika Qur-ani kwamba



"Tuta warejesha dini kuliko walio dini" (95:5)
kayo udio malipo yao watakao fanya maovu ka
pa duniani.

Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye aliandika nukta zote kwa mujibu wa matakwa ya swali, lakini hakutoa maelezo ya kina hivyo kumfanya asipate alama zote 25 za swali hili.

Watahiniwa wengi waliochagua swali hili hawakujibu kwa kufuata matakwa ya swali na kusababisha kupata alama hafifu (0.5 hadi 6). Watahiniwa hawa walitoa Tafsiri na Mafunzo ya Surat Tyn badala na kufafanua mambo yanayoonesha kutukuka na kudunishwa kwa mwanadamu. Kielelezo 1.2 kinaonesha mfano wa majibu ambayo hayakukidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 1.2



1. Kwa jina la Mwenye Zi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu. Naanza kwa kut umia tafsiri na mafunzo ya Surat Tyn (95:4-5)

Naapa kwa tini na Zaituni; Hii ni aya ya kwanza katika sura hii ya Tyn (95:4-5). Aya hii imeonyesha ni jinsi gani mwanaadam wanapaswa kumuabudu Mwenye Zimungu ambayeni mola wake.

Mafunzo tunayoyapata katika surahii ni kwamba mwanaadamu anapaswa kuhapa jambo lililo kuwa halali au lakweli.

Na kwa mlima sinai; Hii ni aya yapili katika surahii ya Tyn (95:4-5). Aya hii imemuonyesha mwanaadamu juu ya ubora wa Allah (s.w) katika dini ya kiislamu.

Mafunzo tunayoyapata kutokana na aya hii, ni mwanaadamu kutambua ubora wa Mola wake na sio ubora wamtu mwingine



Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetumia tafsiri ya Surat Tyn ili kufafanua mambo yanaonesha kutukuka na kudunishwa kwa mwanadamu, alitoa tafsiri ya Surat Tyn na mafunzo yake.

3.1.2 Swali la pili: Qur'an ni Neno la Allah (s.w)

Swali lilihusu mada ya Ithibati ya Qur'an kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu. Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa katika kutathmini hoja za kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu (s.w).

Swali hili lilijibiwa na asilimia 51.6 ya watahiniwa wote. Asilimia 12.8 miongoni mwa waliojibu walipata alama 0, asilimia 49.9 walipata alama 0.5 hadi 7.5 na asilimia 37.3 walipata alama 8 hadi 24. Watahiniwa 2 walimudu kupata alama zote 25.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wengi na ufaulu ulikuwa katika kiwango cha wastani. Watahiniwa waliopata alama za juu katika swali hili waliweza kutoa hoja zilizomo ndani ya Qur'an zinazothibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu (s.w). Hoja hizo ni kutojua kusoma na kuandika kwa Mtume, Qur'an yenyewe kujieleza kuwa ni kitabu cha Allah (s.w), ukiisoma Qur'an kwa makini kuna aya nyingi zinazojieleza kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu alichowashushia wanadamu kuptia kwa Mtume Muhammad (s.a.w), Mtume (s.a.w) kuharakia Wahy wakati wa kuteremshwa akihofia kuwa atasahau, Qur'an kushuka kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka 23, kukosolewa Mtume (s.a.w) ndani ya Qur'an, kutokea kweli matukio yaliyotabiriwa katika Qur'an, mpangilio wa Qur'an, madhui ya Qur'an na mvuto wa ujumbe wake, mwanadamu kushindwa kuandika kitabu mithili ya Qur'an (17:88). Kielelezo 2.1 kinathibitisha ukweli huo.

Kielelezo 2.1

2 Kwa muislamu na kweli anatakiwa kuamini kuwa Qur-ani ni ~~maneno~~ kitabu cha Allah (S.W). Hii ina tokana na kuwepo kwa madai tofauti ya wasio wa islamu dhidi ya Qur-ani. Vipo vipengele vingi katika Qur-ani ambavyo vinathibitisha kuwa Qur-ani kitabu cha Allah (S.W). Baadhi ya vipengele hivyo ni pamoja na;

Kutokujua kusoma na kuandika kwa Mtume (S.A.W). Kwa kuwa Qur-ani imefundishwa au ameletwa ja nayo Mtume (S.A.W), hivyo wako baadhi ya wa kafiri wanadai kuwa Qur-ani ni ya Muhammad (S.A.W). Lakini Allah (S.W) amelipinga dai hili kwa kutuelezea katika Qur-ani yenyewe kuwa Mtume (S.A.W) hakujua kuandika wala kusoma. Hivyo, kwa mtu asiyejua kusoma wala kuandika atawezaje kuwa na kitabu kama Qur-ani? Kwa hili linathibitisha wazi kuwa Qur-ani ni kitabu cha Allah (S.W).

Kukosolewa kwa Mtume (S.A.W) katika Qur-ani. Katika Qur-ani Mtume (S.A.W) amekosolewa katika sura tofauti kama Suratul-Abasa na Suratul-Tahriym. Hii inathibitisha wazi kuwa hii Qur-ani si ya kwake. Kwani itawezekana mtu ajikosoe na kujitia udhaifu au aibu katika maneno yake mwenyewe? Hivyo, hili linathibitisha wazi kuwa Qur-ani ni kitabu cha Allah (S.W).

Qur-ani yenyewe imejielezea kuwa ni kitabu cha Allah (S.W). Kupitia katika Qur-ani kuna aya tofauti ambazo zinathibitisha kuwa hiki kitabu ni cha Allah (S.W). Mfano katika sura ya 25 aya ya kwanza na sura ya 32 aya 2 na 3. Hivyo, hili pia ni kipengele kisha

2 kinachothibitisha kuwa Qur-ani ni kitabu cha Allah (S.W).

Kushindwa kwa mwanadamu kuleta mfano wa Qur-ani. Qur-ani yenyewe imetoa changamoto kwa mwanadamu pamoja na majini kupitia katika aya tofauti kuwa walete mfano wa hii Qur-ani. Mfano katika aya za mwanzo wa Suratul-Baqarah na Suratul-Hud. Ingawa kuna baadhi ya watu walitaka kujaribu kufanya hivyo, lakini hakuna ambaye ameweza hadi leo. Hivyo, kwa kushindwa huku kunathibitisha wazi kuwa Qur-ani ni kitabu cha Allah (S.W)

Mpangilio wa Qur-ani. Qur-ani ni kitabu chenye mpangilio wa ajabu kabisa tofauti na vitabu vyenginé. Mfano kitu ambacho vimetajwa kwa sawa katika Qur-ani basi pia vimetajwa kwa idadi sawa na vile ambacho vimetajwa kwa kiko sawa pia havijatajwa kwa idadi sawa. Mfano Nabii Issa na Nabii Adam wametajwa kuwa ni sawa mbele ya Allah, hivyo na idadi ya kutajwa kwao katika Qur-ani pia ni sawa. Ampapo, Ata'wate wawili wametajwa mara 7 tu katika Qur-ani nzima. Hivyo, kutokana na mpangilio huu wa ajabu wa Qur-ani kunathibitisha kuwa Qur-ani ni kitabu cha Allah (S.W).

Kutokea kwili yaliyotajwa katika Qur-ani. Qur-ani imeelezea matukio mbali mbali ambayo yametokea kwili na mengine yanaendelea kutokea. Mfano Qur-ani imeelezea kuhusu kushindwa kwa dola ya Roma katika kipindi cha Mtume (S.A.W) na ikatokea kwili-



2 Hivyo, kutokana na hali hii inathibitisha wazi kuwa Qur-ani ni kitabu cha haki kinachotoka kwa Allah (s.w).

Kwa ujumla, vipengele viko vingi sana katika Qur-ani ambavyo vinathibitisha kuwa Qur-ani ni kitabu cha Allah (s.w). Hivyo, muislamu anatakiwa awe mwenyeji wa kwelli wa Qur-ani kwa kuisoma, kuifahamu na kufanyia kazi ili aweze kupata malenga ya kiyomo katika Qur-ani.

Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeandika hoja sahihi za kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu (s.w). Kadhalika aliweka nukta za kutosha (sita) na mtiririko wa mawazo yake ulipangika vizuri.

Aidha, baadhi ya watahiniwa walipata alama za chini. Watahiniwa hao waliweza kugusia nukta zinazojaribu kujibu swali. Hata hivyo, walichanganya na maelezo yasiyo sahihi kwa kuingiza maamrisho na makatazo ya Allah, faida na mambo mengine yanayohusiana na Qur'an. Jambo hili lilisababisha watahiniwa wengi kupata alama hafifu na wengine kutopata alama kabisa. Kielelezo 2.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu bila kuzingatia matakwa ya swali.

Kielelezo 2.2



2. Ni kweli kwamba Qur'an ni kitabu cha mwenyezi mungu nathibitishahi li kwa kutoa vipengele vilivyomo katika Qur'an vinavothibitisha dai hili kwamba Qur'an ni kitabu cha mwenyezi mungu kama ifuatavyo :-

Kwanza, kichika Qur'an yaallah (s.a.w) imetuamrisha vyamuachie kusuali na kumwabudu Ili kuyiepusha na mambo machafu na maovu.

Kutoa zakat, pia allah (s.a.w) imetuamrisha kutoa zakat kwani inapotoa zakat unakuwa umejijengea amali nzuri mbele ya allah (s.a.w) na pia hufuti-wa baadhi ya mambo ambayo ulighafi lika na uhawa umemuasi allah.

2 Kuhiji Kwa mwenye uwezo, Ukute
allah amemwamrisha mwanadamu kuhiji
Ha kwa mwenye uwezo kwani kwanza
tukiasa mja na mambo yote machafu alio
yo fanya na kufutiwa dhambi zake
Kufunga mwezi mtukufu wa ramadhani, Allah pia kaitia Qur'an yake ty
kufu amemwamrisha wote kufunga mwezi
mtukufu wa ramadhani kwani pia hutusa
sa mja na kumfanya asifanya mambo ma
chafu na maovu.
Kujisitiri, Ukute Qur'an yetu
h imetwamrisha wote kujisitiri hasa kwa
upande wa kina dada tumewamrishwa kuva
a mawazi yaliyo na stara mbele za watu
Kujisitiri, Ukute Qur'an yetu
h imetwamrisha wote kujisitiri hasa kwa
upande wa kina dada tumewamrishwa kuva
a mawazi yaliyo na stara mbele za watu
Kumwabudu Wazazi wawili,
Allah kaitia Qur'an ~~ya~~ yake, amewatusa kwa
wa heshima wazazi wawili yani baba
na mama kwani hawa ndo mungu wa
hapa duniani na ndo watakuwaka kati
ka sehemu nzuri huko akhera.
Kutokana na mnatathari huo
hapo juu hayo ndo mambo muhimu kwa
mwanadamu kuyafuata na ndo wipengele -
vilivyomo katika Qur'an vinavyothibitisha
kwa Qur'an ni kitabu cha mwenyezi
mungu (s.w.)

Kielelezo 2.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa yaliokuwa kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa huyu alielezea maamrisho mbalimbali yaliyomo ndani ya Qur'an kama kuswali, kufunga, kuhiji na kutoa zaka badala ya kutoa hoja za kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu (s.w).

3.1.3 Swali la 3: Sura Zilizoteuliwa.

Swali lilihusu mada ya Sura Zilizoteuliwa na lilipima ufahamu wa mtahiniwa juu ya kujua tafsiri ya Suratu Nasr (Idhajaa) na namna ya kutumia mafunzo yatokanayo na sura hiyo katika maisha ya kila siku. Swali lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 29.4 ya watahiniwa wote ambapo asilimia 5.6 miongoni mwa waliojibu walipata alama 0, asilimia 9.3 walipata alama 0.5 hadi 7.5 na asilimia 85.1 walipata alama 8 hadi 24.

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni mzuri. Hii inaonekana pale ambapo watahiniwa wengi (asilimia 85.1) wamevuka alama 7.5 ambayo ni kiwango cha chini cha ufaulu kwa swali hili. Watahiniwa waliopata alama za juu waliweza kutoa tafsiri sahihi ya Sura na mafunzo yake. Ufaulu mzuri kwa swali hili ulitokana na maarifa ya kutosha waliokuwa nayo watahiniwa juu ya Suratu Nasri. Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi kwa kuweka maelezo yaliyoendana na matakwa ya swali.

Kielelezo 3.1



3. Suratu Nasr ni sura iliyotere
mshwa makka na ina aya tatu(3)
na ni sura ya 111 katika mpan
gilio wa Qur'ani. Sura hii ni
sura ambayo iliteremshwa na
Mwenye Ezi Mungu kwa kuja
kwa bashiria ushindi waislamu
wote ulimwenguni. Ni sura iliyo
shuka baada ya Hudaibiya na
kabla ya Fat-hu makka. Ifua
tayo ni tafsiri ya Suratu Na
sr (idhaajaa):

Kwa jina la mwenye ezi mung
u mwingi wa rehema mwenye
kurehemu.

1. Pale itapokuja Nasra ya Mwe
nye Ezi mungu (s.w) na mkashi
nda.
2. Mtakapo waona watu wanai
ngia katika uislamu makundi
kwa makundi.
3. Basi ~~a~~ litukuze jina la mola
wako na pia kumutaka msama
ha, kwani ni mwingi wa kupo
kea toba.
Kutokana na Tafsiri hio ya
Suratu Nasr tunapata mafunzo
mbali mbali. Yafuatayo ni ma
funzo ambayo tunaeza pata

3 kutoka na Suratu Nasr. Nayo
ni:-
Tunaji funza kuwa Nusra na
Ushindi unatokana na Allah, Hii
inajionesha wazi pale Allah (S.W)
alipo washiria ushindi hata muda
wa ushindi kufika
Pia licha ya kuwa ushindi u
natokana na Allah lazima tuoneshe
bidii, Hii ni wazi kuwa Allah (S.W)
alibashiria ushindi kwa waislamu
lakini wali pambana kwa hali
na mali mpaka kufikia kwa
pale ambapo Allah (Mwenye Ezi
Mungu) (SW) aliwa akidi
Tuna paswa kulitukuza jina
la Mwenye ezi Mungu (S.W), Hii pia
imeoneshwa katika tafsiri ya Sura
hii kwamba ni dhima yetu
kumtukuza Allah kwa kufanya
yale yote aliyotuamrisha na
kuacha yale yote aliyo tuka
taza.
Tunapaswa kuomba Msamaha
kwa Allah (SW) Pale tu tunapo
kosea, Hii inaoeshwa wazi kw
uye Sura hii kwamba Allah (SW)
hana hasira na wala hana cho
yo kwa yale ambaye amejua
kosa lake na kutubia kwa
kosa hilo.
3 Mafanikio haya patikani bila
jitihada, Hii pia inaonekana kw
aric Waislamu waliji tolea kw
a mali na hali ili kuhakik
isha kuwa Ukhalifa wa Mwe
nye ezi Mungu unasimama.
Hivyo kutokana na Sura
hii tuna pata mafunzo mengi
ambayo kama tutaya tumia
ipasavyo hatutonidi nyuma
na ukhalifa wa mwenye ezi
Mungu (S.W) utasimama.

Kielelezo 3.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa tafsiri sahihi ya Suratu Nasri, pia mafunzo aliyotoa ni sahihi na maelezo yake yamepangika vizuri na kukidhi haja ya matakwa ya swali.

Watahiniwa wenye ufaulu hafifu walijibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuandika tafsiri na mafunzo ya Sura nyingine isiyokuwa Nasri. Zaidi ya hayo, kuna wengine waliandika tafsiri za aya mbalimbali za Qur'an. Watahiniwa walishindwa kujibu swali hili kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya Sura zilizoteuliwa hasa Suratu Nasr. Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vibaya.

Kielelzo 3.2

B Tafsiri

1.) Pindi itakapofika nusura ya mwenyezi mungu
2.) Na akakaremsha baraka kwa dini iliyo nyoka
3.) Na akaka Subira
4.) Kwa waja wake wenye kumwomba msaada
5.) Hakika ya mwanadamu yuko katika hasara

Mafunzo

1.) Mwenyezi mungu anatuhasa kwa katika dini ya Ke iliyonyooka
2.) Tunapaka mafunzo ya kumwa kusubira kwa hakika atayanyoosha mambo yake.

3.) Binadamu anamwa kwingia katika - hasara kwa kutofanya ibada kwa mola wake (Allah)

4.) Mafunzo mtu anamwa kupata nusura dhidi ya vitu vibaya au Uovu

5.) Binadamu anakumbusha kwejua kwake Allah ili kumepo katika njia iliyo nyoo-ka

Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutafsiri na kutoa mafunzo sahihi ya Suratu Nasri, badala yake alichanganya Suratu Nasr na Suratu Asr, na pia alishindwa kutoa mafunzo sahihi ya Sura hiyo.

3.2 SEHEMU B: TAWHIID

3.2.1 Swali la 4: Dini Sahihi

Swali lilihusu mada ya Vigezo vya Dini Sahihi na lililenga uchambuzi wa hoja sita zenye kuthibitisha kuwa Uislamu ndio Dini sahihi. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha hoja sita zinazothibitisha kuwa Uislamu ndio dini sahihi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 25.

Asilimia 44.2 ya watahiniwa wote walijibu swali hili, ambapo asilimia 12.8 ya watahiniwa hao walipata alama 0, asilimia 49.4 walipata alama 0.5 hadi 7.4, asilimia 37.8 walipata alama 7.5 hadi 23.

Ufaulu wa watahiniwa katka swali hili ni wa wastani. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili waliweza kutoa maelezo mazuri yanayoendana na matakwa ya swali kwa kuchambua vizuri hoja zinazothibitisha kuwa Uislamu ni dini sahihi. Hoja hizo ni; Uislamu ni dini ya walimwengu wote na nyakati zote, Uislamu ni dini iliyojengwa juu ya misingi ya ukweli inayoeleza kwa usahihi juu ya muumba, lengo na nafasi ya mwanadamu hapa ulimwenguni na maisha baada ya kufa, Uislamu ni dini yenye taasisi za kujenga na kudumisha utu wa mwanadamu, Uislamu ni dini yenye kusimamia na kupigania haki za binadamu katika jamii, Uislamu ni njia kamili ya maisha, Uislamu ni dini inayotosheleza mahitaji yote ya binadamu ya kimwili na kiroho na Kanuni na sheria za Uislamu zinakwenda sambamba na kanuni na sheria za maumbile yote. Kielelezo 4.1 kinaonesha mfano wa majibu mazuri ya mtahiniwa.

Kielelezo 4.1

4 Dini ya Uislamu ni kule kufuata mfumo na taratibu za Mwenyezi-Mungu (Sw) pekee katika maisha ya kila siku kwa kutekeleza maamrisho na kuacha makatazo yake. Uislamu ni dini sahihi kwa sababu hizi zifuatazo;

Uislamu ni dini ya Mwenyezi-Mungu (Sw) ambae yeye ndie aliemuumba mwanadamu na yeye ndie aliemuekea mfumo wake wa maisha utakuwa ni upi kama Qur-an inavyothibitisha ~~kuwa~~ (3 : 19).

Kwa hali hii dini ya Uislamu imekusanya vipengele vyote vya dini sahihi navyo ni hivi vifuatavyo;

Uislamu ni dini iliyoeleza ukweli wa maumbile: Hapa Uislamu umeeleza chanzo cha mwanadamu kuumbwa kwake kuwa asili yake ni udongo na pia muisho wake kuwa maiti na kufufuliwa (kurejeshwa) tena) ili alipwe kwa kile alichokitenda duniani.

Uislamu pia umeeleza lengo la kuumbwa kwa mwanadamu (2 : 30) na hadhi yake hapa ulimwenguni kuwa yeye ni khalifa wa Mwenyezi-Mungu (Sw). Mambo kama chanzo cha ulimwengu ~~na~~ kuwa ni maji na baadae kuumbwa (kuwekwa) mbingu na ardhi, vyote hivi + vimeelezwa katika dini hii ya Uislamu, dini isiyobakisha chochote katika kufafanua maumbile.

4 **Kanuni na sheria ~~y~~ za Dini ya Uislamu zinaenda sambamba na kanuni na sheria za ~~man~~ maumbile** ya mwanadamu

Hii inathibitika wazi pale sheria kama kuoa inaenda sambamba na maumbile ya mwanadamu kwani inapofika umri maalum mwanadamu huhitaji baadhi ya mahitaji kutoka kwa mwenziwe wa jinsia nyingine na hapo ndio ikawekwa Ndoa.

Pia sheria kama

Muizi akatwe mkono

Mzinifu alie katika ndoa apigwe mawe mpaka afe

Swala ni lazima ili mtu akatazike na mabaya na maovu

Sheria zote hizi na nyinginezo zinaenda sambamba na maumbile ya mwanadamu bila hata ya kukiuka chochote na humuweka mwanadamu sehemu nzuri kabisa inayombakisha ~~kuba~~ kusimama katika lengo lake la kuletwa hapa duniani.

Dini ya Uislamu ni njia ya maisha iliyokamilika: Uislamu haukuacha chochote katika maisha kwani kila nyanja ya kimaisha imeeleza kundani kabisa. Mfano Mambo ya kiuchumi, elimu, siasa na uongozi, afya na maisha kiujumla, vyote hivi vimeelezwa katika Uislamu kupitia kitabu chake Mwenyezi-Mungu (Sw) Qur-an Uiyosafika (na uzushi na uongo).

4 Dini ya Uislamu humtosheleza mwanadamu mahitaji yake: Mahitaji haya ikiwemo kiroho na kimwili.
Uislamu umeeleza nini afanye mwanadamu anapokuwa katika shida na huzuni (awe na subra na mstahamilivu) pia anapokuwa katika raha amshukuru mola wake na kuomba dua.
Pia mahitaji ya kimwili ikiwemo usafi (tohara) na sitara uislamu unatilia mkazo masuala haya. Hii inaonyesha wazi kuwa Uislamu humtosheleza mwanadamu katika mahitaji yake yote.
Uislamu umeweka ibada maabum:
Hii ni kumhakikishia mwanadamu kuwa mbali na sheitani na matashi yake mwenyewe binafsi (mwanadamu) anakaa katika mstari ulionyooka unao takiwa na mola wake (Allah (SW)) Mfano Ibada kama swala, funga, Hijja na Zakka humfanya mwanadamu ~~aw~~ abaki katika lengo lake aliloumbiwa. Ibada zote hizi humfanya akae mbali na maovu, ~~ato~~ awe mchamungu, atakasike na kila machafu yeye na mali yake kwa ujumla.
Uislamu ni dini ya Walimewengu wote na Nyakati zote: Hapa tunaona kuwa Uislamu haukuja kwa kabila fulani tu, au taifa fulani bali umeletwa

4 kwa watu wote rika zote mataifa yote na wala haichagui rangi wala lugha ya mtu. Waislamu watanzania, waislamu wa Makka, Madina, China na Urusi wote uislamu wao ni mmoja hamna tofauti ni ule ule wa Nabii Ibrahim (A.S). Kwa hoja hii wanadamu wanahakikishiwa ukweliwa dini hii na usahibi wake katika maisha ya kila siku, Qur'an (7:156)
Kwa ujumla dini iliyo ya haki mbele ya Mwenyezi-Mungu (SW) ni Uislam na hoja ~~ni~~ ~~zilizotajwa~~ za hapo juu zinathibitisha ukweli huu.

Kielelezo 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa upana na kwa ushahidi hoja zote za kuthibitisha kuwa Uislamu ni Dini ya haki mbele ya Mwenyezi Mungu.

Watahiniwa waliopata alama za chini katika swali hili walishindwa kubaini majibu yasiyo sahihi. Baadhi yao walitoa maelezo kuhusu aina mbalimbali za dini; Kwa mfano, dini ya ukafiri, dini ya ushirikina na dini ya utawa. Kielelezo 4.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa ambayo yalikwenda kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 4.2

4. Bila Shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu (3 : 19)
Hoja sita kuthibitisha aya hii
Dini ni mfumo wa maisha ya ~~kita~~ mwanadamu anaoufuata kila siku
Kuna Dini ya watu, Dini ya Allah
Dini ya Allah (SWT) ni dini ambayo binadamu wameumbwa wamuabudu Allah (SWT) ~~ana~~ kama anavyosema katika Qur-ani ifuatayo
"Bila shaka Sikuwaumba majini na watu ila waniabudu mimi"
(51 : 56)
Dini ya watu ni dini ambayo inafuata mfumo wa maisha ~~ya~~ ya mwanadamu hapa ulimwenguni
Dini ya washirikina ni dini ambayo washirikina wanapenda kutumia dini ya ushirikina kama kufanyia ubaya wao.
Dini ya matakwa ya watu wengine wanaathiriwa na midomo wao hiyo basi ndio hwawezi kufuata dini ya Mwenyezi Mungu
Dini sahihi ni dini ambayo ni ya Allah (SWT) kwa kufuata Qur-ani tukufu ni uthibitisha kuwa dini ya haki ni dini ya Mwenyezi Mungu (SWT) kama inavyosema katika sura (3 : 19)
Dini ya MIMungu ni dini sahihi hapa ulimwenguni kuliko dini yoyote hapa ulimwenguni dini sahihi ni dini ya Allah (S.W.T)
Hiyo kutokana na maelezo ~~ta~~ ya hapo juu bila shaka dini (ya haki) ni mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu (3 : 19)

Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa hoja za kuthibitisha kuwa Uislamu ndio Dini sahihi. Mtahiniwa alitoa maelezo yenye kuelezea aina mbalimbali za dini.

3.2.2 Swali la 5: Shirk

Swali lilihusu mada ya Nguzo za Imani na lilimtaka mtahiniwa kuchambua aina kuu nne za Shirk na kina cha uovu wa Shirk kwa mujibu wa Qur'an. Swali lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 27 ya watahiniwa wote ambapo asilimia 8.4 ya watahiniwa hao walipata alama 0, asilimia 43.6 walipata alama 0.5 hadi 7 na asilimia 48 walipata alama 7.5 hadi 22.

Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa waliofanya swali hili ni cha wastani na wengi wao (58.8) walipata alama kati ya 5 hadi 15. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili waliweza kuchambua aina kuu nne za Shirk kama vile Shirk katika dhati ya Allah (s.w), Shirk katika sifa za Allah (s.w), Shirk katika mamlaka za Allah (s.w) na Shirk katika hukumu za Allah (s.w). Pia waliweza kuonesha kina cha uovu wa Shirk kwa mujibu wa Qur'an kama yalivyo matakwa ya swali. Kielelezo 5.1 ni mfano wa majibu mazuri ya mtahiniwa.

Kielelezo 5.1



5. Shirki ni kujaalia kuwa kuna viumbe wengine mbali na Allah (s.w) ambao wanauwezo wake na ambao wanashirikiana naye katika wengi wa ulimwengu huu. Shirki ina hatara kubwa katika jamii zetu kwanza hupinduwa watu, huleta migogoro na kubeleuana kwa ya watu. Kuna aina kuu nne za shirki ambazo ni shirki katika dhati ya Allah (s.w) katika sifa zake katika hukumu zake, katika mamlaka ya Allah (s.w). Ufuatao ni ufafanuzi juu ya aina nne za shirki na kisha cha uovu wa shirki.

Shirki katika dhati ya Allah, hii ni aina mojawapo ya shirki ambayo watu humshirikisha Allah (s.w) kwa kujaalia kuwa kipo viumbe kingine kama Allah (s.w) kwanye uwezo ~~wa~~ kama wake katika ufanisi wote mfano Mungu, mawaamu mizimu ~~juu~~ juu, majabari, miti mikubwa, kwa kuviomba na kuvinyenyekea kwa kuvitaka msaada. Hivyo hiyo ndiyo shirki ya dhati ya Allah (s.w).

Shirki katika sifa za Allah (s.w) hii ni aina mojawapo ya shirki ambayo watu huvipa viumbe visivyokuwa Alla (s.w) sifa za Allah ambazo hazisitahiki kuvipa pia humpa Allah (s.w) sifa asizozisitahiki mfano huvipa viumbe sifa ya kutoa riziki, kuumba, kufufua, kufisha na sifa nyingineza. Pia humpa Allah sifa asizozitahiki mfano kulala kulakuwa na mengine mengi. Hivyo hiyo ndiyo aina ya shirki ya sifa za Allah (s.w)

Shirki katika Mamlaka ya Allah (s.w) pia na hii ni mojawapo ya aina ya shirki ambapo watu hujipa au huvipa viumbe mamlaka ya Allah (s.w) ambayo havavisitahiki mfano

J Mfano watu hujipa mamlaka ya kutawala ulimwengu wanavyojua wao na wanavyotaka. hujipa
5 mamlaka ya kuwandia watu mfumo wa maisha na kuwandia watu sheria isiyo ya Allah (s.w) mfano katika. Hivyo ndivyo wanavyomshirikisha kupitia aina hii ya shirki katika mamlaka ya Allah (s.w)

Shirki katika hukumu ya Allah (s.w) hii ni aina ya shirki ambayo watu humshirikisha Allah (s.w) kwa kuhukumu kinyume na maamrisho ya Allah (s.w) anavyoelekeza katika kuhukumu. Mfano Allah (s.w) ameelekeza mwizi akatwe mkono, mlevi apigwe bakora ambairi, mzinifu ambaye hajana au kuolewe apigewe bakora mia moja. Na hukumu nyingineza. lakini watu wanahukumu kinyume na hivi. Hivyo hiyo ndiyo aina ya shirki ya hukumu ya Alla (s.w)

Ifuatayo ni kina cha uovu wa shirki kwa mujibu wa Qur-an. Kama ifuatavyo.

Kwa mujibu wa Qur-an kina cha uovu wa Shirki ni hivi ifuatavyo

Shirki ni dhulma kubwa kuliko zote, kumshirikisha Allah (s.w) ni dhulma kubwa kuliko zote hivyo. Allah (s.w) atutahadharisha na dhulma hiyo.

Shirki ni dhambi kubwa kuliko zote isiyo sameheka mbele ya Mwenyezi mungu pindi mtu huyo akifa bila kuleta toba. Hivyo shirki haitasamehewa kama anavyosema katika Qur-an (4:48)

Shirki hufuta mema yote yaliyotangulia pindi mtu anapomshirikisha Allah (s.w) hivyo tujiepushe na shirki maana inafuta mema yote tuliyoyatangulizapia tulete toba.

Allah (s.w) ameandaa adhabu kali na kubwa kwa wanaomshirikisha ~~Qur-an~~ kama anavyobainish



Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua aina kuu nne za Shirk. Pia alitoa maelezo mazuri kuhusu kina cha uovu wa Shirk kwa mujibu wa Qur'an.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengi walijibu kinyume na matakwa ya swali jambo lililosababisha kupata alama za chini, ambapo zaidi ya nusu ya watahiniwa (asilimia 52) hawakufikia alama 7.5 ambayo ilikuwa ufaulu wa chini kwa swali hili. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha aina nne za Shirk. Zaidi ya hayo, watahiniwa wengi walishindwa kujua maana ya kina cha uovu wa Shirk kwa mujibu wa Qur'an na hivyo kushindwa kabisa kujibu sehemu hii. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri.

Kielelezo 5.2



gia 'Amri zao hivyo wanadamu wanamua
si Allah katika dhati kwa kumshirikisha. Hiv
yo wanadamu wanamshirikisha Allah kwa kupi
ga ramli (bao) yaani kuaguliwa. Hivyo wanada
mu wanamshirikisha Allah katika dhati

Shirk katika nafsi hii ni aina ya shirk
ambayo mwanadamu anatumia nafsi yake viba
ya kwa kumshirikisha Allah Mfano kupiga
bao ni shirk kubwa inayomshirikisha Allah
katika Masuala ya Ushirikina. Mwanadamu
anatumia njia ya kumuamini mwanadamu mw
enzake zaidi ya Allah

Shirk katika Umbile la mwanadamu.
Ni aina ya shirk ambayo mwanada anamshrik
sha Allah kwa kumkosoa jingi alivyo umba vitu
na watu katika ambile alilopendekeza yey

5 Allah (s.w) mwanadamu anamshrikisha Allah
kwa kudhani kuwa Allah ana upendeleo ka
tika kuumba kwake. Hivyo mwanadamu ana
pandikiza shirk katika maumbile. Mfano
ulimwengu wa sasa akina dada wanamuasi
Allah kwa kujibadilisha rangi za ngozi zao

Mwisho shirk ni dhambi kubwa ambayo
ataangamia mwanadamu atakayejaribu kum
shirikisha Allah kwa kumkufuru Mwenyezi
mungu juu ya makatazo yake. Aliyoyakataza
katika Qur-an na Sunnah.

Kielelezo 5.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyetoa maelezo tu kuhusu mada ya Nguzo za Imani inayoelezea Shirk na hivyo kwenda kinyume na matakwa ya swali. Pia mtahiniwa hakueleza chochote kuhusiana na kina cha uovu wa Shirk.

3.2.3 Swali la 6: Nguzo za Imani

Swali lilihusu mada ya Kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu na watahiniwa walitakiwa kutathmini taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku kwa Muislamu. Swali lilikuwa na jumla ya alama 25.

Asilimia 21.3 ya watahiniwa wote walijibu swali hili ambapo asilimia 26.9 ya waliojibu swali hili walipata alama 0. Aidha, asilimia 50 walipata alama 0.5 hadi 7 na asilimia 23.1 walipata alama 7.5 hadi 23.5.

Ufaulu wa watahiniwa kwenye swali hili ni wa kiwango cha chini. Watahiniwa wengi (asilimia 50) wamepata alama za chini (alama 0.5 hadi 7) kwenye swali hili na hivyo ufaulu wa swali hili haukuwa mzuri. Hii ilitokana na maelezo yao kwenda kinyume na matakwa ya swali kwa kueleza kazi na sifa za Malaika bila ya kueleza taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku. Watahiniwa wengine (asilimia 26.6) wamepata alama 0 kwa kutokuelewa mada ya swali hili kwani hawakuandika zaidi ya utangulizi ambao pia haukuwa sahihi. Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri kwa mujibu wa matakwa ya swali.

Kielelezo 6.1

6 Malaika, ni viumbe ambayo wameumswa kwa
nuru ya mwenyezi mungu ~~a~~ mfalme wa viumbe vyo
te duniani na akhera. Malaika hawaonekani katika
macho ya viumbe kama binadamu. Kutokana na swa
li linavyojieleza ~~k~~ zifuatazo ni ufafanuzi wa
taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya
kila siku ni kamavile,

Kutorewa kutoa roho za binadamu, ni kitendo
au mkatabba maalumu kati ya mja na mola wak
e ukifikia hakuna budi kukimbia kufa. Mfano wa
malaika Israili, yeye kazi yake kuwa ni hii k
atika maisha ya kila siku.

Kuwadhibu watu makaburini, ni kuwapatia
watu walioko katika makaburi 'adhabu kali sa
na kama wikuwa si mchamungu, kwa mfano ni
malaika Munkar na Nakir kazi yao watu ni
hii tu katika makaburi pamoja na kuuliza maswal

Huwa wanaandika mema na mabaya yote anaf
anyo mwanadamu. Hii ndiyo kazi ya malaika hawa
katika maisha yetu ya kila siku, kwa mfano
ukiswali na kufanya toba kwa siku hiyo wandik
a vilevile ukizini, ukanywa pombe nayo pia hvandika

Huja duniani kila ipikapo wiku wa manane
kuja kuangalia nani anafanya nini na nani ana
omba kitu gani na mfumo mzima wa maomsi yako
Mfano mtu akiswali swala za wiku na akaomba
kwa mola wake jamso analolitaka basi malaika
hawa hufikisha ujumbe wako wa Allah (s.w)

Vile hushusha wahyi, malaika ~~mikaal~~, Israfil
kazi yake kubwa ni kuteremsha uzima kwa mana
bii wa Allah (sw) na hana hata usaguzi au
kazi nyingine isipokuwa hii. Kwa mfano mfupi

Kielelezo 6.1 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa ambaye alieleza kazi mbalimbali za Malaika badala ya kueleza taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku ya Muislamu.

Watahiniwa wachache wenye ufaulu mzuri waliweza kueleza kama yalivyo matakwa ya swali ya kutathmini taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku. Watahiniwa hawa waliweza kutoa hoja sita na kuzifafanua vizuri. Kielelezo 6.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyejibu kulingana na mahitaji ya swali.

Kielelezo 6.2

6 Malaika ni viumbe wa Allah (sw) ambao wa
meumbwa kutokana na nuru na ambao hawana
hiari katika kuabudu ni lazima wafanye ibada
lengo la kuumbwa Malaika ni kumuabudu Allah sw
Katika kuamini Malaika kunaweza kukatwa taathira
nyingi kwa Mwanadamu, Miongoni mwa Taathira
hizo ni

Kwanza, Kumfanya mwanadamu kujiepusha na
kumshirikisha Mwenyezimungu na viumbe visivyoone
kana kama Majini na Malaika. Kuamini malaika
kunampelekea mwanadamu kujua kuwa Allah sw am
eumba viumbe ambavyo havionekanwi na kusaba
bisha binaadamu kuacha Kumshirikisha Mlmungu
na viumbe hivyo kwa kuwa anajua vyote ni vium
be vya Allah (sw)

Pili, Kufanya juhudi ya kumuabudu mola
wake ili awe Khalifa wa Allah (sw) na hadhi ku
liko ile ya Malaika. Mwanadamu atakapokuwa
anajua kuwa kumbe Malaika ni viumbe wa
Allah na ambao wanamuabudu Allah, basi ataji
tahidi kufanya ibada ili alifikie lile lengo la ku
letwa kwade duniani na kuwa na hadhi ya kuwa
Khalifa wa Allah (sw)

Tatu, Kumfanya mwanadamu ajitahidi kufa
nya mambo mema kwa kuwa na yakini kuwa
siku ya malipo kutakuwa na malaika watakao
waonibe msamaha wale mizani zao za thawab
zitakazokuwa nyepesi kuliko za dhambi. Hii ina
pelekea kumfanya mwanadamu kufanya khen
na kuwa na matumaini kuwa Malaika nimi
ongoni mwa viumbe watakaoshufaiya watu siku

6 ya malipo ambapo watu watakuwa katika hali
ya udhalili

Nne, Kuwa tayari kupigania dini ya Allah(sw)
kwa kujua kuwa Allah(sw) atawaleta Malaika am
bao watawasaidia. Mwanadamu atakuwa hana
wasi wasi juu ya jambo la kupigania dini yake
kama Allah(sw) alivyowaremshia waislamu jes
hi la Malaika katika vita vya ~~uhudi~~ badri.

Tano, Kujiepusha kufanya maovu kwa kuwa
na yakini kuwa kuna Malaika wanaoandika
amali za binaadamu. Kuamini malaika kuna
mfanya mwanadamu kuacha maovu na mamb
yote machafu kama vile kutukana, kisengeny
kuzini nk na kumfanya aogope kuyafanya k
wa kuwa atakuwa anakumbuka kuwa kuna
malaika wanaoandika amali za wanadamu

Sita, Kumfanya mwanadamu vitendo vizuri
ili kuja kupata nafuu wakati wa kutolewa ~~roho~~
roho. Mwanadamu atajitahidi kufanya mema
na vitendo vizuri, kuwa anajua akifanya ma
mbo mema basi atapata nafuu ama machung
u ya kutolewa roho na Malaika kuliko atakap
kuwa anafanya vitendo vioovu.

Kwa hiyo, kuamini malaika ni nguzo
katika nguzo za Imani na ambazo humpele
kea mwanadamu kujichungo na kila anac
hokifanya na kumpelekea kuishi maisha
ya kumcha- Allah (sw) katika kipindi cho
te cha uhai wake atakaoishi hapa duniani.

Kielelezo 6.2 kinaonesha namna mtahiniwa alivyojibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali na kueleza hoja zote sita.

3.3 SEHEMU C: FIQH

3.3.1 Swali la 7: Nguzo za Uislamu (Swala)

Swali lilihusu mada ya kusimamisha Swala na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kuchambua sababu sita zinazowafanya wengi wanaoswali kutofikia lengo la Swala. Swali lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 54.7 ya watahiniwa wote ambapo asilimia 2.2 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 42.1 walipata alama kati ya 0.5 hadi alama 7 na asilimia 55.7 walipata alama 7.5 hadi 22.5.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wengi na ufaulu wake ni wa kiwango cha wastani. Watahiniwa wachache waliopata alama za juu waliweza kuchambua sababu zinazowafanya wengi wanaoswali wasifikie lengo la Swala. Sababu hizo ni; wengi hawalijui lengo la kusimamisha Swala, wengi hawatekelezi masharti na nguzo za Swala ipasavyo, wengi hawaswali kwa unyenyekevu (khushui), wengi huswali kwa kujionesha (ria), wengi hawadumu katika Swala, wengi huswali kama ni ada waliorithi katika jamii au wazee lakini hawajishughulishi kupata ujuzi au taaluma ya kutosha juu ya Swala na kutosimamisha Swala za jamaa ipasavyo. Kielelezo 7.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa yanayoendana na matakwa ya swali

Kielelezo 7.1

7. Swala ni nguzo ya pili miongoni mwa nguzo za Uislamu, jambo hili ni miongoni mwa mambo yaliyotiliwa mkazo sana ndani ya Uislamu kwani jambo la mwanzo kutesabiwa mwanadamu siku ya mwisho basi ni swala lakini pia utenile wapo wale ambao wanaswali lakini hawafikii lengo hilo la Swala; miongoni mwa yanayopelekea kutofikia lengo la swala ni haya yafuatayo:

Wengi wanaoswali hawajui lengo la swala ; kama ilivyo lengo la swala ni kumuepusha mja na maovu na machafu lakini baadhi ya wale ambao wanaswali hawajui lengo hili na wanajikuta wanaswali tu pasina kujua lengo hasa linalowapelekea wao kufanya ibada hii ya swala hivyo kwa kuto kujua kwao lengo hili la swala huwapelekea kutojikia lengo hilo la swala na kujikuta wanaswali tu.

Wengi wanaoswali hawahifadhi swala zao ambazo huwapelekea kutojikia lengo la swala unakuta mtu anaswali tu bila ya kuihifadhi swala yake anaswali basi tu ilimradi na yeye awe ameswali pasina kufuata nguzo na sharti mbali mbali za swala hivyo huwapelekea wao kutojikia lengo hilo la swala

Wengi wanaoswali hawaswali ka unyenyekevu (khushui) hivyo huwapelekea wao kutojikia lengo la swala kwani unakuta mtu anaswali lakini hajajituliza kifikra wala kimwili mtu anaswali huku anajikuna mwengine anaswali anawaza mambo mengine hivyo ukosefu wa khushui ndani ya swala hupelekea wengi wanao tekeleza ibada hii kutojikia lengo la swala.

7. Wengi wanaoswali hawasimamishi swafu za jamaa ipasavyo utakuta mtu asubuhi ameswali jamaa tena msikitini halafu adhuri hayupo hivyo kwa kutosimamisha kwa swafu bizi za jamaa kama ~~[illegible]~~ inavyostahiki ipasavyo basi hupelekea wengi wao wanaoswali kutojikia lengo la swala kama linavyotakiwa lijikiwe na yule anayeswali ambayo ni kumuepusha mja na maovu na machafu.

Wengi wanaoswali wanaswali kwa ria (kujionyesha), hivyo hupelekea watu kutojikia lengo la swala kama inavyotakiwa kwa mfano uta kuta mtu anaswali ili mtu fulani au watu fulani wamuone kuwa na yeye anaswali lakini hawali kwa Ikhlasi pia kuna wanaoswali ili wapate au wapewe kitu fulani kwa kuficha yote hii ni ria hivyo hupelekea watu kwa kutojikia lengo la swala.

Wengi wanaoswali hawathungi ma sharti ya swala; kama vile stara unakuta mtu anaswali lakini hayupo stara kama inavyojuli kana kwa stara kwa mwanamke ni mwili mzima kasoro uso na viganja vya mikono hivyo hivyo kwa mwanaume ni kati ya magoti na kitovu hivyo basi uta kuta mtu anaswali pengine nywele kidogo zinaonekana kwa mwanamke au kutoelekea kibla yote haya hupelekea lengo la swala kutojikiwa na wengi ambao wanaoswali.

Ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha kuwa anatekeleza sharti na nguzo zote za swala kama inavyotakiwa ili iwe sababu ya mtu huyo kuweza kujikia lengo la kuswali kwake ambalo ni kumuepusha mja na mambo ambayo ni machafu na maovu.

Kielelezo 7.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kutoa sababu sita pamoja na maelezo yanayojitosheleza. Zaidi ya hayo, mtahiniwa aliandika utangulizi mzuri pamoja na hitimisho.

Kwa watahiniwa waliopata alama za chini, majibu yao yalikuwa kinyume na matakwa ya swali. Wengi wa watahiniwa hao walieleza maovu mbalimbali yanayofanywa na baadhi ya wanaoswali kama vile kuzini, kuiba, kulewa na kusengenya; majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo 7.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 7.2



7. **Swala**:- Ni kitendo cha kumcha mungu ipasavyo na pia inatakiwa kusmaliwa kama ilivyoamrishwa na mwenyezimungu kwa niaba ya maja wake wa duniani; Mfano wa swala hizo ni Adhuhuri, Alasiri pamoja na Ishaa Naanza na hoja kama ifuatavyo:-

Kutoacha matendo machafu:- Hii inaonyesha pale mwanaadamu anapoamua kuanza kusmali lakini akiwa anasmali badomambo yake machafu anayo basi swala yake haifiki popote mpaka uache matendo maovu aliyokataza Mwenyezi mungu na kufuata ali

Kutokuisoma Qur'an ipasavyo:- Hii ni sababu kubwa kwa sababu humtezi kusmali kama huijui Qur'an vizuri mana kuna sura za kusoma kuna dua za ~~kusoma~~ kuomba baada ya swala ili mwenyezimungu aipokee swala yako.

Kutokujua masharti ya swala:- Hii ni sababu kwa sababu wanaadamu wengi wanasmali lakini ~~mas~~ hamajui kama swala inamasharti yake hivyo utakuwa hujafikia lengo la swala.

Kutokujua vipengele vya swala:- Hii ni sababu kubwa kwa sababu wanaadamu wengi wanasmali hamajui unaanzaje wala unamalizaje au utakuta mwanaadamu mwengine akiinama hajui pia ashike wapi wala akisimama hajui pia mikono inakaaje.

Hivyo basi tunatakiwa tusome Qur'an vizuri ili tujue kusmali, dua za kumuomba mwenyezi mungu ili akuepushie na matendo maovu uliyokuwa ukiyafanya au usiyaf

Kielelezo 7.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa ambaye alieleza mambo ambayo mtu anayeswali anapaswa kuyaacha badala ya kueleza sababu zinazowafanya wengi wanaoswali kutofikia lengo la Swala.

3.3.2 Swali la 8: Ndoa katika Uislamu

Swali lilihusu mada ya familia ya Kiislamu na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kueleza masharti yanayopaswa kutekelezwa na muolewaji katika ndoa ya Kiislamu. Swali lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 29.2 ya watahiniwa wote. Miongoni mwa watahiniwa waliojibu swali hili, asilimia 11.4 walipata alama 0, asilimia 61.3 walipata alama 0.5 hadi alama 7 na asilimia 27.3 walipata alama 7.5 hadi 23.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha chini. Watahiniwa wengi hawakuwa na ufaulu mzuri ambapo karibu asilimia 61.3 ya watahiniwa hawakufikisha alama za wastani (7.5) ambazo ziilikuwa ndiyo ufaulu wa chini. Watahiniwa wengi waliojibu vibaya, walishindwa kuelezea masharti sita yanayopaswa kutekelezwa na muolewaji katika ndoa ya Kiislamu, wao walieleza nguzo za ndoa ya Kiislamu na wengine walieleza majukumu ya mke kwa mumewe. Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa maelezo yasiyosahihi.

Kielelezo 8.1



8	Ndoa ya kiislamu ni makubaliano kati ya mwa
	na-ume na mwanamku kuungana kuwa mke na mu-
	me kwakufuata utaratibu na sheria za kiislamu.
	Kuna mashartiambayo anatakiwa aweameyatekeleza
	muolewaji katika ndoa ya kiislamu nayo ni
	Aweametimiza umri wa kuolewa kwamwanam-
	ke yeyote wa kiislamu haluusiwi kuolewa mpaka awe
	ametimiza umi wa miaka 18 na kuendelea ndiyo
	atakuwa amefuata taratibu anazopaswa kutekele-
	za muolewaji katiku ndoa ya kiislamu



Kielelezo na 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetaja masharti ya jumla ya ndoa ya Kiislamu badala ya masharti yanayopaswa kutekelezwa na muolewaji katika ndoa ya Kiislamu.

Watahiniwa wachache waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na uelewa mzuri wa mada ya ndoa kwa kuweza kujibu kwa ufasaha. Watahiniwa hao waliweza kueleza masharti yanayopaswa kutekelezwa na muolewaji katika ndoa ya Kiislamu kama vile asiwe katika ndoa ya mume mwingine, asiwe katika eda ya mume mwingine, asiwe ni maharimu kwa

mume anayemuoa na asiwe katika kuhirimia Hija au Umra. Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali.

Kielelezo 8.2

8 Ndoa ni maingiliano ya kisheria katika ya mke na mume. Muoleweji anapaswa atekeleze majukumu yapatayo katika ndoa ya kiislamu.

Asiwe katika eda: Ili ndoa ya kiislamu isihi, muoleweji anatakiwa asiwe katika eda ya kupewa au kuachwa na mume mwenginę asiyekuwa anaetaka kumuoa.

Mfano: Ikiwa muwanamke yupo ndani ya eda ya kupewa na mume wake, hapaswi kuolewa na mtu mwengine yeyote mpaka amalize eda yake hiyo.

Asiwe katika ndoa nyengine: Muwanamke anaetaka olewa hapaswi kuwa katika ndoa nyengine kwani sheria ya kiislam inamtaka muwanamke wa kiislam kuolewa na mume mmoja tu kwa wakati mmoja.

Mfano: Muwanamke ambae hajaachika katika ndoa yake, lakini akaolewa na mtu mwengine bali kwa hatika ndoa hiyo ni batili.

Asiolewe na maharimu wake: Muoleweji hatakiwi kuolewa na maharimu wake (mtu ambae hapaswi kumuoa) na akifanya hivyo bali ndoa hiyo siyo sahihi.

Mfano: Kaka, ~~dad~~ muwanawe, baba yake na mjomba wake.

Asiwe katika vazi la Ihram ya hija: Ni haramu muwanamke kuolewa bali ya kuwa ameva aa vazi la kuhiji (Ihram).

Mfano: Muwanamke akiwa katika hija hatakiwi kuol

8 wa mpaka alivue vazi la Ihram alilovaa (mpaka amalize hija).

Aolewe kwa ridhaa yake : Muolewaji anatakiwa aridhie na akubali kuolewa bila ya kulazimishwa kwani bila ya ridhaa ya muolewaji, patakuwa hapana ndoa yoyote.

mpano : Ndoa hufungwa pale ambapo muolewaji hucema "ndio nimekubali" ndipo ndoa itakubalika.

Awe na akili timamu : muolewaji anatakiwa aolewe akiwa ana akili timamu na awe muelewa wa ndoa yenyewe.

mpano : Aliyerukwa na akili japo kwa muda mpaja hafai kuozeshwa kwaza mpaka ziridi akili zake kwani akiolewa itakuwa kaolewa bila ya idhini yake.

Masharti haya yote endapo yatatekelezwa, ndipo ndoa ya Kiislam itaweza kukubalika na kuweza kufikiwa lengo lake.

Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu mazuri. Mtahiniwa alitaja na kuelezea masharti sita yanayopaswa kutekelezwa na muolewaji katika ndoa ya Kiislamu. Aidha, mpangilio wa insha ni mzuri ukiwa na utangulizi na hitimisho.

3.3.3 Swali la 9: Swala ya Maiti

Swali lilihusu mada ya mambo ya lazima kufanyiwa Maiti wa Kiislamu na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa juu ya utekelezaji na utaratibu wa Swala ya Maiti hatua kwa hatua. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 9.7 ya watahiniwa wote ambapo asilimia 6.2 miongoni mwa watahiniwa hao walipata 0. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 64.5 walipata alama 0.5 hadi 7, asilimia 28.9 walipata alama 7.5 hadi 20 na asilimia 0.4 walipata alama 21 hadi 23.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wachache, na alama zao zilikuwa za chini. Watahiniwa wengi waliojibu swali hili walishindwa kutoa maelezo ya Swala ya Maiti hatua kwa hatua, na badala yake walitoa maelezo yanayohusiana na Swala ya Maiti bila kufuata Utaratibu. Hali hii ilisababisha watahiniwa wengi kupata alama za chini na wengine kutopata alama. Baadhi yao walitoa maelezo yanayohusiana na mambo muhimu yakufanyiwa Maiti wa Kiislamu ambayo ni kukoshwa, kuvikwa sanda, kuswaliwa na kuzikwa. Majibu ya namna hii yalikuwa ni kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maelezo yenye kukidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 9.1

9 Imamu, ~~ikifuative~~ ikifuatiwa na Maamuma-
kisha maiti.
Ili swala ya maiti itekelezeke zifua-
tazo nia hatua jinsi ya kutekleza swala-
ya maiti
Kuoshwa, Maiti lazima aoshwe
haraka mapema iwezekanavyo na pale-
anapooshwa ~~kula~~ huwa lazima dua ita-
mkwe. Na maiti wa kiume anaoshwa
na waislamu wanaume na maiti wa kike-
anaoshwa na waislamu wa kike
Kuvalishwa sanda, Maiti anapo-
malizika kuoshwa lazima avalishwe-
sanda. Hivyo katika maiti ya kiume
inatakiwa vibande vitatu na katika-
maiti wa kike inatakiwa vipande
vitano. Baada ya hapa maiti anata-
kiwa aapambwe kwa vile vinavyotakiwa
Kuswaliwa, maiti lazima
anapomalizika kuvalishwa sanda kina-
chofuata ni kuswaliwa ili kuwa-
~~taray~~ tayari katika kurejesheva mahala
pake. Hapa imamu anamuombea-
dua maiti ili kuwa tayari katika
kuzikwa ikifuatiwa na maamuma.
Kuzikwa, Maiti lazima
anapomalizika kuswaliwa kinachofuata



9 ~~Watu~~ ni kuzikwa, hapa tayari kaburi-
limesha chimbwa hivyo maiti kuwa taya-
ri katika kuzikwa. Hapa wanatangu-
lia maamuma katika kumchukua maiti
na kuanza safari ya kumpeleka kabu-
rini. Kabla ya kuzikwa imamu wana-
tangulia wawili kindani ya kaburi na
kicha kumpokea maiti kisha kuweka
udongo hapo tayari maiti imeshazikwa.
Ki kinachofuata ni kuomba dua ili-
kuwa shukuru wale ~~wat~~ umati walio-
huduria katika kushiriki ~~mas~~ a mazishi.
Hivyo hizo endizo hatua anazota-
kiwa kufanyiwa maiti katika kutekele-
za swala ya maiti.

Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejikita katika kuelezea mambo muhimu ya kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, badala ya utekelezaji na utaratibu wa Swala ya Maiti hatua kwa hatua.

Watahiniwa wachache waliopata alama za juu waliweza kutaja na kuelezea utaratibu wa utekelezaji wa Swala ya Maiti hatua kwa hatua, kwa kupanga vipengele vyake kwa mujibu wa utaratibu ulio sahihi. Utaratibu huo ni pamoja na kutia Nia ya kumswalia maiti, kuleta takbira nne kusoma Suratul-Fatha, kumswalia Mtume (s.a.w), kumuombea dua maiti, kuwaombea dua waislamu wote na kutoa salaam. Kielelezo 9.2 kinaonesha namna mtahiniwa alivyoweza kujibu swali vizuri.

Kielelezo 9.2



9 SWALA YA MAITI. Ni moja
miongoni mwa mambo ya wajibu
kufanyiwa maiti wa Kiislamu. Swala
hii huwa na kusimama lakini haina
rukuu wala sijida katika
kuswaliwa maiti, yeye pamoja
na wanaomswalia hujipanga kama
ifua tavyo.
MAITI: Maiti atapangwa

mbele ya wanaomshwalia (imamamu na Maamuma. Wakiwa ni mchanganyiko wa kike na kiume. Maiti wa kiume watapangwa mbele kutoka kwa imamu kisha watafuata wale.

IMAMU (Anaesalisha), Anakaka mbele ya maiti waliopangwa kutoka mume kwenda mke kama kuna mchanganyiko. Ni sunna kwa Imamu kukaa karibu na kichwa kwa maiti mume na kwa mke kukaa maeneo ya tumbo.

MAAMUMU (Wanao Swalishwa) wanafuata nyuma ya imamu.

NAMNA SWALA INAVYO SWALIWA

HATUA.

(i) Imamu pamoja na maamuma wake watatia nia na kuleta takbira ya kwanza. (Maamu lakima afanya hivi baada ya imamu hali ya kutochelewa sana)

(ii) Watasoma Suratul Fatha kila mmoja kimya kimya (kuitikia Aamin ni sunna)

(iii) Wataleta takbira ya pili baada ya imamu (Maamu)

(iv) Wote Imamu na maamuma watamswalia mtumu.

(v) Wataleta takbira ya tatu

(vi) Kisha watamuombea dua maiti

"Ewe mola mnehemu maiti wetu huyu" kwa kiarabu. Na vile vile wataongezee. Ewe mola usitujaalie matatizo baada ya kuondoka kwake

(vii) Kisha wataleta takbira ya nne.

(viii) Kisha watawaombea dua waislamu wate kwa ujumla

(ix) Kutoa salamu ya kwanza.

Hivyo ndio namna ya kuwapanga maiti, imamu na maamuma, na hatua kwa hatu tunavyo iswali swala ya "MAITI". Kuna sunna vile vile katika kumswali a maiti miongoni mwazo ni

(i) Kusoma ~~Suratul~~ - ! Sura nyengine baada ya Suratul-Fatha.

(ii) Kuitikia Aamin.! Baada ya Suratul- Fatha.

(iii) Safu ziwe katika idadi ya witri

(iv) Kutoa salamu ya mwisho.

Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa kufuata matakwa ya swali. Mtahiniwa aliweza kutaja na kuelezea utaratibu wa utekelezaji wa Swala ya Maiti hatua kwa hatua, kwa kupanga vipengele vyake kwa utaratibu ulio sahihi.

3.4 SEHEMU D : TAREKH

3.4.1 Swali la 10: Historia ya Uislamu Kipindi cha Makhalifa Wanne Waongofu

Swali lilihusu mada ya Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa Wanne Waongofu na lilipima uwezo wa mtahiniwa kuchambua njia nne zilizotumika kuwaingiza madarakani Makhalifa Wanne Waongofu na mafunzo yanayopatikana kutokana na njia hizo. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 25.

Asilimia 9.5 ya watahiniwa wote walijibu swali hili, ambapo asilimia 44.8 ya waliojibu walipata alama 0, asilimia 46.9 walipata alama 0.5 hadi 7 na asilimia 8.3 walipata alama 7.5 hadi 21.

Swali hili ndilo lililojibiwa na watahiniwa wachache katika mtihani huu na ufaulu wa watahiniwa hao ni hafifu ambapo watahiniwa wengi (asilimia 44.8) walipata alama 0. Ufaulu hafifu katika swali hili ulitokana na watahiniwa wengi kutokuelewa matakwa ya swali, hivyo kujibu kinyume na maelekezo ya swali. Watahiniwa wengi walieleza sifa na historia za maisha ya Makhalifa wanne Waongofu, badala ya kueleza njia zilizotumika kuwaingiza madarakani. Hii ilisababisha baadhi ya watahiniwa hao kupata alama 0 kwa kuwa majibu yao hayaendani na matakwa ya swali. Pia watahiniwa waliopata alama za chini (alama 0.5 hadi 7) hawakuwa na maarifa ya mada ya Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa wanne Waongofu na hivyo kutojibu vizuri hasa sehemu ya pili ya swali ambayo ilimuelekeza mtahiniwa kutoa mafunzo yanayopatikana kutokana na njia zilizowaingiza madarakani Makhalifa wanne Waongofu. Kielelezo 10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.

Kielelezo 10.1

10 Ziyotaro ni njia zilizo tumika ku waingiza madarakani makhalifa wanne wa engofu wa mtume (s.a.w) na mafunzo ma wili tunayopata kutokana na njia hizo.

Walikuwa maswahaba wa mtume (s.a.w); hii ni njia moja wapo iliyo tumika ku waingiza madarakani makhalifa waongofu kwa sababu walikuwa ni marafiki wa Bwana mtume Muhammad (s.a.w) hii ni njia mojawapo iliyo tumika kuwa ingiza madarakani.

Walimsaidia mtume (s.a.w) kati ka kuandika hadithi; pia hii ni njia moja wapo iliyotumika kuwaingiza mada rakani makhalifa hao kwa mfano Abu bakari, Ommar, Othman na Ally wali saidia kuandika hadithi na kuhifadhi Qur-an.

Walikuwa ni wapole; pia hii ni njia moja wapo iliyotumika kuwa ingi za makhalifa hao madarakani kwa sa babu walikuwa wapole, wanyenyekevu na wenye huruma kwa watu pia wali shi rezuni na mtume (s.a.w) funzo tunalo lipata wa Islamu tuwe wapole na wanyenyekevu.

Walikuwa waaminifu kwa watu; hii ni njia moja wapo iliyotumika kuwa ingiza madarakani makhalifa hao kwa sababu walikuwa ni wanyenye kevu pia waaminifu kwa watu. funzo tunalo lipata kwao ni kuwe wanyenye



10. kewa pia kuwe wapde na wenyeku
toa ushauri mzuri kwa watu.
Walikuwa waislamu, pia hii ni
njia iliyo changia kufumika katika
kuchaguliwa kwa Makhalifa wanne wa
ongofu wa mtume (s.a.w) kwa Saba
bu walikuwa ni waislamu mafunzo
kunayo yapata hapo ni kwamba kuwe
waislamu kwa mayo mmoja kwani kuna
weza kupata bahati kama hino.
Kwa kumalizia, Makhalifa wanne
waongofu wa Mtume (s.a.w) ni kama
Abubakar Swidik, Ommar bin hatwab,
Othman na Ally bin Abutwalib. hawa
dio makhalifa waliokuwa wanamsima
mo na msikamano katika dini ya
Allah (s.a.w) na dio Sababu yaku
Chaguliwa kwao.

Kielelezo 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua njia zilizowaingiza madarakani Makhalifa wanne Waongofu, bali alieleza sifa za masahaba.

Watahiniwa wachache tu ndio walioweza kujibu swali hili kwa mujibu wa matakwa ya swali na kupata alama za juu. Watahiniwa hao waliweza kueleza njia nne zilizowaingiza madarakani Makhalifa wanne waongofu na pia waliweza kutoa maelezo mazuri kuhusiana na mafunzo mawili yanayopatikana kutokana na njia hizo. Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kueleza kwa mujibu wa matakwa ya swali.

Kielelezo 10.2

10: Khalifa ni kiongozi wa waumini anayeongoza
kwa niaba ya Allah (s.w). Baada ya kufariki M
tume walioongoza dola ya kiislamu ni Abu Bakar (r.a)
10. Ummar (r.a), Uthmani (r.a) na Alii bin Abu
Talib (r.a). Viongozi hawa walifuata nyayo za
Mtume (s.a.w) waliwekwa madarakani kwa nama
zifazotofautiana bila kuvunja sheria za kiislamu
katika kuwapata viongozi. Katika njia hizi zilizotumika
kuwamamba mengi ya kuji dmza. Njia zilizotumika
kuwaingiza madarakani Makhalifa wanne wa Mtume
(s.a.w) ni hizi zifuatazo:

Njia ya mgendekezo; Njia hii ilitumika katika
kumuingiza madarakani Khalifa wa kwanza, Abu Bakar
(r.a), Baada ya Mtume kufariki kabla hajazikwa Wais
lamu walikutana kwenye ukumbi ili kufanyiana etekaa
Shikilia nafasi ya Mtume, Muhajirina walipendekezo kiongo
zi atoke ansar na Ansar walipendekezo atoke Muhajirina
Muhajirina alipendekezwa Umar, Abu Bakar na Ubaidi, hatima
ya Umar (r.a) na Ubaidi (r.a) walikempendekezo Abu Bakar
na pale pale walikampa mkono wa baiya (ahadi ya utii) na
waislamu wengine wote walikatenya huyo

Njia ya kufuata; kufuata pia na njia ilyo
tumika kupata viongozi katika uislamu kama ilivyotumiwa
na masuwaheba. Njia hii ilotumika kumpata. au
kumueka madarakani Ummar (r.a) Khalifa wa pili
wa Mtume (s.a.w). Hii ni baada ya Abu Bakar (r.a)
kumteua Ummar (r.a) ili ame Khalifa baada yake. Ba
hii ya Abu Bakar (r.a) ili kubaliwa na waislamu wote
na hatimaye walimpa ahadi ya utii Ummar (r.a) kama
kiongozi wa dola baada ya kufariki Abu Bakar (r.a).

Njia ya kuchagulwa; Hii ni njia ambayo
ilitumika kumpata Khalifa wa tatu, Uthmani. Ummar
(r.a) alivyokuwa anakaribia kufariki, aliteua watumbe
wa Shura sita akiwemo Uthmani, Alli na Talha
aliwaagiza kuwa kiku tatu baada ya yeye kufariki

10. Wachaguzi wengine ili mmoja wao awe Khalifa aongoze dola ya Kiislamu. Baada ya kutawala Umar (r.a) Wajumbe hawa walikumchagua Uthmani bin Affani (r.a) kuwa Khalifa wa tatu wa dola ya Kiislamu ilipo chukua madaraka.

Njia ya Mapinduzi; Hii ni njia ambayo imetumika kumuweka Madarakani Alii bin Abutwalib (r.a) Madarakani kama Khalifa wa nne wa dola ya Kiislamu. Alii aliweka madarakani baada ya kuuliwa Uthmani na kikundi cha watu walikuwa wanamtaka Alii kuwa Khalifa badala ya Uthmani, hii ndio sababu ni kaita njia hii kama njia ya mapinduzi. Kwa hapo Alii aliweka madarakani kwasababu na kitimaye dola ya Kiislamu ilianza kuvunjika kwa mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Lakini Alii bin Abitwalib alibaki katika uchamungu wake bila kutetereka ila waumini wengine ndio walikuwa na matatizo ya kutomthamini Kiongozi kilu sababisha si kosa la kiongozi.

Hizo ndio njia zilizo tumika kumpata makhalifa hawa wanne waongofu katika madaraka. Kuna mengi ya kujifunza kutoka katika njia hizi. Matunda ambayo tunayapata kutokana na njia hizi zilizo tumika kumweka madarakani Makhalifa hawa wanne ni haya yafuatayo:

Kuwa heshima viongozi; Kutowa heshima viongozi ni chanzo cha machafuko matukuwa fani katika dola. Tumeona kuwa waumini walikuwa hawawa heshimu viongozi mwishowake ikasababisha mapigano ya yenyewe kwa wenyewe na kumwaga damu Zanduga zao, hili lisingetokea kama wangewa heshimu viongozi walio pamoja daraka.

Kiongozi ni lazima awe na elimu na mchamungu

Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi kwa kuweza kueleza njia zilizowaingiza madarakani Makhalifa wanne Waongofu. Njia hizo ni kuteuliwa, kupendekezwa, kuchaguliwa na mapinduzi. Pia mtahiniwa aliweza kutoa maelezo yaliyopangika vizuri kuhusiana na mafunzo yanayopatikana kutokana na njia hizo.

3.4.2 Swali la 11: Mkataba wa Hudaibiyah

Swali lilihusu mada ya Ushindi wa Waislamu (Fat-hu-Makkah) na lililenga kumpima mtahiniwa katika stadi za maarifa na uchambuzi ambapo swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua matokeo ya kihistoria yanayodhihirisha ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya Mkataba wa Hudaibiya. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali lilijibiwa na asilimia 16.3 ya watahiniwa wote ambapo asilimia 21 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 51.2 walipata alama 0.5 hadi 7 na asilimia 27.8 walipata alama 7.5 hadi 21.5.

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni hafifu ambapo watahiniwa wengi (asilimia 72.8) walipata alama za chini ambapo miongoni mwao, asilimia 21 walipata alama 0. Watahiniwa waliopata alama za chini walionekana kutokuwa na maarifa ya mada ya Ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya Mkataba wa Hudaibiya, hivyo walipata alama chache sana. Hii ilitokana na maelezo hafifu waliyoyatoa yakiambatana na matukio machache ya kihistoria yanayodhihirisha ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya Mkataba wa Hudaibiya. Watahiniwa waliopata alama 0 walionekana kutokuelewa matakwa ya swali na kushindwa kutoa majibu sahihi. Wengi wao walichambua vipengele vya Mkataba wa Hudaibiya badala ya matukio ya kihistoria, wengine walieleza historia ya tukio la Hudaibiya na wengine walieleza mambo yatakayosababisha maendeleo ya Dola Kiislaamu majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambayo hayajakidhi matakwa ya swali.

Kielelezo 11.1

11: Dola ya kiislamu ni sheria ya kiislam
iliyo wekwa na mwenyezimungu na kuamri
sha watu kufuata ~~hizyo~~ hizo sheria za
kiislamu kwa sababu sasa kila muislamu
anafuata utaratibu aliowweka Allah (S.W)
na una waongoza katika ~~nyiradi~~ nyiraka zao za
kila siku asubuhi hadi jioni na hata usiku.
Zifuatazo ni sababu zinazoonesha
ushidi wa dola ya kiislamu baada ya
mkataba wa Hudaibiya
Dola ya kiislamu ina ushahidi
tosha kwa mwenyezimungu kwa sababu
watu walifundishwa uislamu na dola
ya kiislamu kusimamishwa na Mtume
Mohamadi (S.A.W) kwa ajili ya kuongoza
maisha yao ya kila siku, na dola ya
kiislamu imesaidia waislamu wengi
kujua uislamu na kuendeleza kwa wa
watu ambao hawataki kufuata uislamu
kamili kama aliyo amrisha mwenyezimungu
Dola ya kiislamu ina ushahidi
pale ambapo watu wataokuwa na Imani ya
kweli toka moyoni kwa mfano kunabaadh
ya makafiri walienda juu angani kumta
futa mwenyezimungu wakidai kuwa wana
sikia mwenyezimungu yupo mbiguni basi waka
enda huko mbinguni kumtafuta mwenyezimung
basi walipopanda huko mbinguni na vifaavyao
vya kupima kwa ajili ya kumuona mwenye
zimungu lakini hawakuweza kufaniki wa na
walipopanda huko basi mudawa swala
ukafika sasa cha ajabu mtu aliyekuwa

11. huku chini au ulemwenguni aliweza kuto
azana kwa kujulisha watu kuwa sasa ni
muda wa swala basi hadi huko kwa
wale makafiri waliokuwa wanadai uislamu
sio dini sahihi basi makafiri wanafafuta
hii Sauti inatoka wapi huku juu mbona
watu wanaoishi hata mmoja na wala
hatuya muona mungu? wakapima kutafuta
hawa watu wako wapi? waliwakosa basi
baada ya hiyo waliposhuka basi walio
kuwa na imani wakaamini kuwa uislamu
ndio dini ya kweli na wale ambao hawa
kuamini hawa kuweza kusilimu na kuwa
waislamu basi wale waliokubali kusili
mu na kuwa waislamu mungu aliwase
mehe na wale ambao hawa kusilimu mungu
hakuweza kuwa sameha kwa sababu walika
taa kufuata utaratibu wake.

Dola ya kiislamu ita kuwa na
ushahidi pale ambapo watu wata kuwa
msimamo mzuri katika dini yao ya kiisla
mu na hata wange shawishiwa na shetani
hawangeweza kushawishika kwa sababu wana
msimamo mzuri wa dini yao na kufuata
utaratibu ulio wekwa na mwenyezimungu
kuwa watu wote wanatakiwa kumfuata
mwenyezimungu jinsi aliyowaelekeza katika
vitabu vyake vitukufu.

Dola ya kiislamu itashida pale
ambapo watu wata kuwa wana soma na
kufundisha Qur'an tukufu hapo wataku
wa wamemtekeleza mwenyezimungu mashari

Kielelezo 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea matukio ya kihistoria yanayodhihirisha Ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya Mkataba wa Hudaibiya na badala yake ameelezea mambo yatakayosababisha kukua au kushinda kwa dola ya kiislamu.

Watahiniwa wachache walipata alama za juu, ambao kwa namna fulani waliweza kuchambua matukio ya kihistoria yanayodhihirisha Ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya mkataba wa Hudaibiya. Matukio ya kihistoria yaliyochambuliwa na watahiniwa ni pamoja na kuleta mwingiliano kati ya makafiri wa Makka na Waislamu wa Madina, Waislamu kupata fursa ya kulingania Uislamu, kusimamishwa kwa vita ambapo kulisababisha kukua kwa uchumi wa Dola ya Kiislamu na kutekwa Makkah toka mikononi mwa Makafiri wa Kikureishi. Kielelezo 11.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali kwa kutoa maelezo sahihi.

Kielelezo 11.2



11. Mkataba wa hudaibiya ni mkataba uliofanywa baina
ya waislam wa madina na Maquraishy wa makka katika kitongo
ji cha Hudaibiya mbali kidogo na mji wa makka katika mwaka
wa 6 A.H. Mkataba ulisainiwa ili kuwazuia waislam kutofanya
Umrah na kuwaamuru kuwa warudi Madini. Kiongozi upandewa
waislam alikuwa ni mtume (s.a.w) na upande wa maquraish 'alikuwa
Ubaidah. Mkataba huu ulikuwa kama kuwanyonya waislam lakin
baadae ulipelekea ushindi wa dola ya Kuslam kupitili matukio
yafuatayo.
Kutekwa kwa mji wa Makka (fat-h makka). Hayo
yalikuwa matunda ya mkataba huu ambapo waislam waliweza ku
fanya hijjah ambayo ilikuwa ya kuaga katika mwaka uliofuata
7 A.H. Mtume (s.a.w) alikuwa takribani na waislam 10,000
Hivyo walingia katika mji wa makka kupitia sehemu mbali mbali
za mji huo lisi ikapelekea maquraiysh kushindwa kuwazuia
Hii ilipelekea waislam na dola ya Kuslam kushinda.
Waislam waliweza kuutangaza uislam wao kwa
vitendo. Kabla ya mkataba huu watu wa madina walikuwa na
uadui na watu wa makka lakini baada ya kusainiwa mkata
ba huu uliwafanya waislam waruhusiwe kwenda madina hivyo
waliweza kufanya da'wa kwa vitendo vyao vilivyokuwa vizuri
zilivyo wavutia wa maquraish wa makka mpaka nao wakaslim. Hii
ilipelekea waislam kushinda kwa kuwa watu wengi waliongezeka ka
tika dini ya Kuslam.
Waislam walipata uhuru wa kufanya biashara
na wasiokuwa waislam katika mji na vitongoji vya makka
Huu ulikuwa ni ushindi mwingine kwa kuwa waislam
waliweza kujiendeleza kuchumi ambapo walipata kipato
kikubwa ambacho kiliwasaidia katika kuendesha ha
rakati na kuimua dola ya Kuslam.

11. Majemedali wengi wa Maquraish au w
Kiquraysh walisilimu jambo lilisababisha waislam kuwa
na nguvu na kuweza kuwelekea ushindi katika maqura
ysh walishinda miongoni mwao ni Khalid bin walid am
baye alikuwa ni Shujaa Sana kuwa uislam ukawa umepata
nguvu na kupelekea kushinda kwa kushindo na kuwagu
u ya dini nyingine kipindi hicho.

Kisilimu kwa wafalme mbali mbali kulotka
Sehemu tofauti tofauti za bara la Arabu. Wafalme walweza
kusilimu kwa kuwa walikiishiwa ujumbe wa uslam. Lakini
wapo wengine walioukataa na kuwa wajumbe walio
waletea ujumbe huo. Lakini wengine walikubali kama vile
Najash wa Habesh na akawa muislam.

Waislam walweza kuutanga uslam ndani na
nje ya Arab. Katika miongoni mwa vipengele vya mkataba
wa hudaibiya kipengele cha Sita kinasema kuwa pasiwe hawta
kwa kipindi cha miaka 10. Hii ilwapa waislam nafasi ya ku
tangaza uslam Sehemu nyingine tofauti na Arab. Sehemu
walizopeleka ujumbe ni kama Habesh, Misri na Sham. baadh
ya viongozi walisilimu lakini wengine walikataa.

Dola ya kislam ilweza kupanuka na kuwa
kubwa mpaka nje ya Arab. B N baada ya mkataba hu
wa hudaibiya ambapo dola ya kislam ilipopanuka na
kuweza kusambaa mpaka nje ya Arab ambapo mtume S.a.w
alweza kutuma magavana wakuweza kuuendesha uslam
na kusfundisha miongoni mwa magavana walikuwa ni
Muadh bin Jabar alyeenda Misri. Hiki kipengele kinaonesha
kuwa au kindhihirisha uhindi wa uislam na waislam.

Mambo haya yalyotokea baada ya Mkataba wa
Hudaibiya yanaonesha kuwa mkataba huu ulikuwa sio
wa kuwanyonya kama walivyo kuwa wameona mawataba
bali ulikuwa ni uhindi ambao Allah (s.w) alikuwa ameuandaa

Kielelezo 11.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye aliweza kuchambua matokeo ya kihistoria yanayodhihirisha Ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya Mkataba wa Hudaibiya kwa kuandika nukta muhimu zenye kuakisi matakwa ya swali.

3.4.3 Swali la 12: Dhana ya Uislamu juu ya Historia

Swali lilihusu mada ya Dhana juu ya Historia katika Uislamu na lilipima uwezo wa mtahiniwa kutathmini mambo sita muhimu kwa Waislamu wa leo kujifunza Historia ya Uislamu. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 25.

Swali hili ndilo lililojibiwa na watahiniwa wengi katika karatasi ya pili ambapo asilimia 62.1 ya watahiniwa wote walijibu swali hili. Asilimia 21 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 67.8 walipata alama 0.5 hadi 7 na asilimia 11.2 walipata alama 7.5 hadi 23.5.

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni hafifu sana ambapo asilimia 88.8 ya watahiniwa wameshindwa kufikia alama 7.5 ambayo ilikuwa ufaulu wa chini. Ufaulu huu hafifu ulitokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kwa watahiniwa wengi na hivyo kushindwa kuchambua umuhimu wa Waislamu wa leo kujifunza Historia ya Uislamu. Pia watahiniwa wengi (asilimia 21) walieleza Historia za Mitume tofauti. Wengine walieleza hoja za kuwepo Mwenyezi Mungu kwa kupitia maisha ya Mitume na wengine walieleza amri mbali mbali walizopewa Mitume katika Uislamu. Watahiniwa hao walipata alama 0. Kielelezo 12.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeeleza historia ya mitume kinyume na maelekezo ya swali.

Kielelezo 12.1

12. Na kwa yakini tuliwatuma mitume kablayao. W
engine katika hao Tumekusimulia na wengineh
tukusimulia (40:78) kwa kutumia aya (ma
mbo sita muhimu kwa waislamu wa leo kujifu
nza historia ya uislamu. nikama inavyofuat
Historia ya nabii yussuf ni historia ili yojaa
maskitisho makubwa. kwa waislamu wa zama
hizi ni vigumu kufuata historia hii kwa m
fano nabii yussuf alilelewa katika nyumba
ya kifalme yenye kila raha ya staarehe il
maskitiko makubwa ni pale mke wa mfalm
e alipompenda na kuingia shahwa kwana
bii yussuf na kushindwa kuvumilia. bila shaka
tuliona jinsi nabii yussuf alivyo kataa na kumt
a (Bibi Zuleikha) ili kujinusuru na maovu ya
le. Waislamu wasasa wengekua wao wenge
kua tayari na kusherehekea kwa sualali
Historia ya nabii mussa. Zama zamabii
mussa mfalme Firaauni akiwauwa watoto
wakiume na kuacha watoto wa kike hatim
ae ukaja wahyi wa kupinduliwa mfalme-
na nabii mussa kulelewa katika nyumba ya
mfalme. laiti ingekua ni zama za sasa w
aislamu wengekua tayari na kujiingiza kat
ika ukafiri ili wapate pesa na maliza makafi
ri.
Historia ya nabii Ibrahim. Nabii huyu ali
shushiwa wahyi ili kumuuwa mtoto wake Is-
mail na alikua tayari kufanya hivyo kwam
toto wake. Zama zasasa ingetokea hivyo mtu
engepinga na kumkosoa Allah (S.W).



12 Historia ya nabii adam. Nabii adam aliingiape
peni pamoja na mke wake (hawa) ila walito
lewa kwa kosa la kula tunda mmoja tuAla-
baadae akarudi kwa m.mungu ili apate-
kusamehewa.
Historia ya Nuh. historia hii katika kijiji-
cha nuhu waislamu walikuwa kidogo sana
na nabii nuhu alifanyiwa unyama na mak
afiri pale Alipoamrishwa na mola wake kuten
geneza jahazi na makafiri wakaamua kwe
nda kuweka kinyesi kwenye jahazi. ila baa
dae wakayasafisha wenyewe.
Historia ya nabii suleiman. Nabii suleiman-
aliamrishwa na Allah ili apeleke ujumbe kwa
makafiri kuhusu uislamu. Na kufikia hatima-
mkubwa wa waislam kuslimu. Nabii huyu al
ipewa ujuzi wa kuzungumza na hata ndege
Hayo ndiyo mambo yanayotakiwa waislamu
wajifunze nayo. ili wapate shufaiwa nai ku
fuata mila za manabii waliopiata kabla-
yetu.

Kielelezo 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea historia ya Mitume mbalimbali kinyume na maelekezo ya swali.

Watahiniwa wachache sana walikuwa na ufaulu mzuri ambapo majibu yao yalikidhi matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi mambo muhimu kwa waislamu wa leo kujifunza Historia ya Uislamu. Mambo hayo ni; kuonesha kuwepo kwa Allah (s.w) na mamlaka yake juu ya binadamu na viumbe vingine vyote, kuonesha asili na hadhi binadamu juu ya viumbe wengine hapa duniani, kukumbusha

lengo la kuumbwa kwa binadamu na namna ya kulifikia, kuonesha namna Allah (s.w) alivyowaneemesha wanadamu ili kuweza kumuabudu sawasawa, kuonesha madhara ya kutofuata mwongozo wa Allah (s.w), kutoa hamasa ya kupambana na matwaghuti kwa kuzingatia walivyofanya mitume na watu wema waliopita, kuwezesha watu kujitathmini na kuongeza jitihada za kusimamisha Uislamu katika jamii na kutoa fursa ya kujifunza toka kaumu zilizopita na kuchukua tahadhari kabla ya kupata madhara yaliyozipata kaumu hizo. Kielelezo 12.2 Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alijibu kwa kufuata matakwa ya swali.

Kielelezo 12.2



12 Historia ni jumla ya matukio yaliyopita na vile
vile yaliyo fanyika katika kipindi cha nyuma kama
vile matendo mazuri, mema, mabaya na mambo meng
mbali mbali. Historia hutuelezea jinsi mitume watu
na wafuasi wengine walivyokua wakishi na kuu
simamisha Uislamu katika ulimwengunu vilevile
hutuonyesha matendo mabaya yaliyo fanywa na
binadamu kwa mfano Historia ya Nabii Musa na
firauni, jinsi firauni alivyokuwa mbaya na kujipa
yeye uungu. katika Uislamu ni muhimu kujifunza
historia kwa sababu zifuatazo:
Hutuonyesha kuwepo kwa Allah na mamlaka

12 yake kwa wanadamu, Waislamu ni muhimu sana kujifunza historia kwa sababu inatuonyesha dhahiri kuwepo kwa mwenyezi mungu na mamlaka yake kwetu kwa mfano. katika vita vya badri alivyo pigana Mtume muhammad na waislamu wengine dhidi ya makureishi Ambapo kundi la waislam wa liliku wa kidogo lakini la makureishi liliku wa ni kundi kubwa na lenye silaha lakini katika vita hivyo waislamu ndio walikuwa washindi japokuwa walikuwa ni wachache. Hii inatuonyesha dhahiri kwamba mwenyezi mungu anitoa msaada mkubwa sana kwa waja wake kwa kuwapangwa zaidi.

Hutuonyesha madhara ya kutofuata muongozo wa allah, vile vile kujifunza historia kwa waislamu ni jambo muhimu sana kwa sababu inatuonyesha madhara ya kutofuata muongozo wa Allah kwa mfano katika historia ya Nabii Musa na firauni inatu onyesha kwamba firauni hakufuata muongozo wa allah ~~ete~~ kwa kumkana kabisa na kujitia yeye ni mung u lakini mwisho wa siku alipata madhara makubwa sana ya kutariki bahrini akiwa na kundi lake la watu wengi. pindi alipokuwa akimfuata musa

Hutuonyesha asili na hadhi yetu juu ya viumbe wengine hapa duniani, katika kujifunza historia kwa waislamu ni muhimu kwa ~~a~~ sababu inatuonye sha kwa sisi ni asili yetu nini na hadhi yetu juu ya viumbe vyote. Asili ya mwanadamu hutuonyesha kwamba ni udongo na hadhi yetu ni kumiliki vitu vyote vya hapa duniani kwa sababu mwanadamu ameperewa wezo mkubwa wa upeo na akili ya kuweza kuvitawala vitu vyote vya hapa duniani.

12 Hutukumbusha juu ya lengo la kuumbwa kwetu, vilevile katika kujifunza historia hutukumbusha kwamba lengo la kuumbwa kwetu ni kumwabudu mwenyezi mungu kama walivyokuwa wakiabudu mitume wetu na wafuasi wao. Hivyo basi watu hatunabudi kusoma sana historia ili kufahamu lengo letu la kuumbwa.

Kujitathimini na kuongeza jitihada za kusimamisha haki na uadilifu kama walivyofanya mitume na watu wema, Historia tunajifunza jinsi mitume walivyokuwa wakisimamisha haki kwa watu wote bila upendeleo kwa mfano. Mtume wetu Muhammad (S.aw) alikuwa akisimamisha haki kwa watu wote bila kujali udini na vilevile alikuwa na uadilifu na aliamini wa na kila mtu kama vile alikuwa anawapa watoto majina mazuri, alikuwa anawatetea wanyonge.

Hutuonyesha namna Allah alivyowaneemesha watu ili tuweze kumuabudu ipasavyo, vilevile ni muhimu sana kujifunza historia kwa sababu hutuonyesha dhahiri jinsi alla alivyowaneemesha watu wa kabla yetu ili sisi tupate kumwabudu ipasavyo bila kipingamizi chochote. Kwa mfano katika hadithi za mtume zimekuwa zikituonyesha jinsi mtume alivyoneemeshwa kutokana na jitihada zake za kumwabudu na kumwomba mwenyezi mungu.

Historia ni jambo muhimu sana katika maisha ya waislamu kwa sababu humfanya muislamu awe msimamishaji wa haki katika jamii, Huwafanyu watu wampende sana mwenyezi mungu kwa kumuabudu ipasavyo. Hivyo basi waislamu hatunabudi kuendelea kujifunza historia ipasavyo kwa kuzingatia mafunzo na maamrisho ya Allah.

Kielelezo 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza mambo sita muhimu kwa Waislamu wa leo kujifunza Historia katika Uislamu. Pia mtahiniwa alikuwa na mtiririko mzuri wa mawazo katika kueleza hoja zake.

4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila swali umewasilishwa katika makundi makuu matatu ambapo ufaulu umezingatia asilimia 30 au zaidi kwa kila swali, hivyo waliopata alama kati ya 0 hadi 29 ufaulu wao ni hafifu na umeoneshwa kwa rangi ya nyekundu kwenye jedwali. Watahiniwa waliopata alama kati ya 30 hadi 49 ufaulu ni wa wastani ambao umeoneshwa kwa rangi ya njano kwenye jedwali na waliopata kati ya alama 50 hadi 100 ufaulu ni mzuri ambao kwenye jedwali umeoneshwa kwa rangi ya kijani (rejea kiambatisho).

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2014 ni wa kiwango cha wastani. Tathmini iliyofanyika katika karatasi ya kwanza na karatasi ya pili inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa ni wa kuridhisha katika karatasi ya kwanza ikilinganishwa na ufaulu katika karatasi ya pili. Katika karatasi ya kwanza, mada zilizofanywa vizuri zaidi kuliko nyingine ni mada za *Sunnah na Hadithi*, *Fiqh* ikifuatiwa na *Qur'an* ambapo mada ya Tarekh ilifanyika kwa kiwango cha wastani. Mada ya *Tawhiid* ndiyo iliyofanyika vibaya kwa kupata alama za chini kwa watahiniwa wengi. Kwa karatasi ya pili, mada iliyojibiwa vizuri ni *Sura Zilizoteuliwa*, ikifuatiwa na mada ya *Kusimamisha Swala* ambapo mada iliyofanyika kwa kiwango cha wastani ni *Vigezo vya Dini Sahihi*. Kwa upande mwingine mada zilizofanyika vibaya ni *Historia ya Uislamu kipindi cha Makhalifa Wanne Waongofu*, *Historia katika Uislamu* na *Sura Zilizoteuliwa.*

Uchambuzi uliofanyika kwa kuangalia majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada za *Sunnah na Hadithi, Qur'an* (Sura zilizoteuliwa) na *Fiqh* (kusimamisha Swala). Hata hivyo, watahiniwa wengi walikuwa na uelewa mdogo wa mada ya *Tarekh* (Dhana ya Historia katika Uislamu na Mkataba wa Hudaibiya) na mada ya *Tawhiid* (Kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu). Watahiniwa kuandika majibu yasiyoendana na matakwa ya swali, kutoa majibu ya kubahatisha, ni kielelezo kinachodhihirisha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kwa baadhi ya mada. Pia watahiniwa walionesha uwezo mdogo wa kujibu maswali ya kuoanisha vipengele kutoka orodha mbili tofauti pamoja na maswali ya kujaza nafasi zilizo wazi. Kwa ujumla mada iliyofanyika vizuri ni mada ya Sunnah na Hadithi na mada iliyofanyika vibaya ni mada ya Tarekh.

5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango kwa ufaulu katika somo la Elimu ya Dini Kiislamu, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wajitahidi kufundisha na kumaliza mada zote za muhtasari ili kutoa fursa kwa wanafunzi kujiandaa kikamilifu kukabiliana na swali lolote kutoka katika mtaala wao.

(b) Wanafunzi wajengewe tabia ya kujisomea vitabu vya kiada na ziada vya Elimu ya Dini ya Kiislamu ili kuwandaa kwa mujibu wa muhtasari na kuwawezesha kuwa na maarifa ya kutosha kujibu maswali hasa ya kujieleza.

(c) Pamoja na Sura zilizochaguliwa, ni muhimu wanafunzi wajengewe tabia ya kuisoma Qur'an nzima mara kwa mara ili kujiwekea msingi imara wa taaluma ya dini.

(d) Watahiniwa tarajali wapewe mazoezi mengi ya aina mbalimbali ili kuwajengea umahiri wa kutambua matakwa ya swali na uwezo wa kutoa majibu sahihi.

MCHANGANUO WA MADA ZILIZOFANYIKA VIZURI NA HAFIFU SOMO LA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU CSEE 2014

Karatasi ya Kwanza

Na.	Mada	Nambari ya swali	Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi	Maoni
1	Sunnah na Hadithi	1	70.4	Vizuri
2	Fiqh	4	70.1	Vizuri
3	Qur'an	2	53.7	Vizuri
4	Tarekh	5	46.7	Wastani
5	Tawhiid	3	9.4	Hafifu

Karatasi ya Pili

Na.	Mada	Ufaulu wa Kila Swali		Asilimia ya Watahiniwa waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi	Maoni
		Nambari ya Swali	Asilimia ya Ufaulu		
1	Qur'an	3	85.1	45.2	Wastani
		2	39		
		1	11.		
2	Fiqh	7	55.7	37.4	Wastani
		9	29.3		
		8	27.3		
3	Tawhiid	5	48	36.3	Wastani
		4	37.8		
		6	23.1		
4	Tarekh	11	27.8	15.8	Hafifu
		12	11.2		
		10	8.3		